# *Huduma Yangu Mpya*

Vema, Ndugu Neville. Asanteni, ndugu.

2 Habari za asubuhi, marafiki. Bila shaka ni majaliwa kuwa hapa asubuhi ya leo, maskanini. Wakati . . .

3 Tayari tumepakia mikoba yetu sasa, na tunangojea ule mkutano mkubwa kuanza huko San Jose, juma hili, huko—huko San Jose, California. Tutaondoka mara moja baada ya ibada, kuelekea Pwani ya Magharibi. Kisha tutakuwa huko chini Coconut Gardens kwa yapata siku mbili, pia, Bwana akipenda, pamoja na Wafanyabiashara Wakristo. Nasi tunatarajia wakati mzuri sana katika Bwana, kwenye Pwani ya Magharibi. Wana makanisa themanini na mawili katika udhamini, na mashirika yote mawili ya San Joaquin, na hayo mabonde kote kwenye Pwani ya Magharibi. Na kwa hiyo tuko kwenye viwanja vya maonyesho kule. Iwapo baadhi ya marafiki zenu, mwajua, ambao wangetaka kuhudhuria baadhi ya hizo ibada, tungefurahi kukutana na marafiki zenu na—na jamaa zenu.

4 Nasi tunatarajia. Nina ukaguzi mkubwa zaidi . . . matarajio, asubuhi ya leo, na karibu mkutano wowote niliopata kuwa nao, kufikia sasa. Kwa sababu, ninaamini ya kwamba tuko kwenye mkesha wa jambo fulani linalokaribia kutukia. Nimelitarajia kwa muda mrefu. Nami ni—ninaamini ya kwamba tuko papo hapo ukingoni mwake sasa, kwa ajili ya jambo fulani, ambapo Mungu atawasaidia watoto wake wadogo kuendelea mbele njiani.

5 Mnajua, Biblia ilisema, ya kwamba, "Adui anapokuja kama mafuriko, Roho wa Mungu atainua kiwango dhidi yake."

6 Basi Mungu anapolipatia Kanisa Lake baraka, nao wanaendelea mbele na baraka hiyo kwa muda mrefu sana mpaka inakuwa ya kawaida kwa ulimwengu, ndipo wanaanza kuiharibu. Ndipo Roho wa Mungu huingia na kuinua kiwango tena, ndipo kunatokea uamsho ama kitu fulani.

7 Nayo matumaini yetu makuu ni haya, ya kwamba, moja ya siku hizi, Roho wa Mungu atamtuma Yesu Kristo duniani tena, ndipo itakuwa kamilifu basi. Hicho kitakuwa ndicho kiwango halisi.

8 Sasa wao wanasimama tu, kote ku—kutani na kadhalika, na kote jengoni. Nilikutana na mtu akiingia, nilipoliegesha gari langu, naye akasema . . . Nikasema, "Nitaliacha limesimama hapa, pamoja na ufunguo, ndipo unaweza kuondoka wakati wowote utakao."

9 Akasema, “Vema, nilijaribu kuingia. Nisingeweza kupata nafasi ya kusimama.”

10 Nalo kanisa letu ni dogo kupita kiasi kwa ajili ya mkutano. Lakini nikiondoka asubuhi ya leo . . . Nasi tulilitangaza Jumapili iliyopita, kuhusu kuwa hapa, na tungekuja kuwaombea wagonjwa. Na kuwapa maagizo juu ya yale tuliyokuwa tumeona yakitukia. Na kumekuwako na mengine, kwa neema ya Mungu, yaliyoongezewa kwake, kwa ajili ya asubuhi hii.

11 Sasa, tumehubiri, na wengine mbele yetu, juu ya Kuja kwa Bwana kulikokaribia, kule Kuja kulikokaribia. Nasi tunaamini kwamba kunazidi kukaribia. Bila shaka, kunazidi kukaribia, siku baada ya siku. Lakini kama tungeweza kusimama na kuwazia, ya kwamba, moja ya siku hizi, mtalisikia kwa mara ya mwisho, halafu Bwana Yesu atakuja.

12 Dunia yote, miti, maumbile yote, watu, Kanisa, kila kitu, kinaugua, kinaomboleza, kinashikilia, kikiingojea siku hiyo, Kuja Kwake. Maumbile yanajua ya kwamba yata—yataacha kuteseka wakati huo. Nao watu wanajua wataacha kuteseka wakati huo. Mauti yatapoteza mshiko wake wa mwisho, nalo kaburi na kuzimu zitamezwa katika ushindi.

13 Nilifurahi sana, asubuhi ya leo, kukutana na maskini mchungaji huyu hapa aliyetuchezea muziki na akaimba, kutoka Sellersburg. Mmoja wa hao ndugu amekuwa akizungumza juu ya uamsho unaoendelea huko juu. Nami nadhani tayari wameutangaza, na kadhalika, kwa hiyo hilo ni sawa kabisa. Bwana na awabariki huko juu, katika kila jitihada wanayotoa, ndilo ombi langu aminifu, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

14 Sasa, Neno la Bwana ni la thamani sana kwetu. Tunajua hilo. Kwa hiyo, leo hii, ninaamini ya kwamba tuko karibu sana na Kuja kwa Bwana, nayo mashamba yana mahitaji mengi sana.

15 Nimekuwa tu nikizungumza na baadhi ya ndugu. Ninaamini sehemu kubwa ya huduma yangu itaelekezewa nchi za ng’ambo sasa. Tunapanga kwenda Afrika, mara baada ya Krismasi, na kuingia huko Australia na nyingi ya sehemu hizo. Bwana anatenda kazi sasa na kutufungulia njia. Tumekuwa na mialiko, kote ulimwenguni, kwa muda mrefu. Nasi huenda tukaweza kuifanya hiyo mara baada ya Krismasi sasa, iwapo nyote mtatuombea.

16 Sasa hapa mbele yangu ninalo Neno la Mungu limefunguliwa. Sasa nimefungua kurasa, kwa sababu, kimwili, na kwa msaada wa Mungu, ninaweza kufanya hivyo, kuifungua Biblia. Bali sina uwezo wa kuyafungua yaliyomo. Kunaye Mmoja tu anayeweza kufanya hivyo, na huyo ni Mungu, peke yake. Yeye Ndiye aliyeliandika, kwa Roho Wake Mtakatifu, na Yeye Ndiye pekee anayeweza kutufungulia Biblia. Nami ninatumaini ya kwamba Yeye ataifungua mioyo yetu tunapolisoma, na atalifanya lijulikane kwetu.

17 Nitazungumza kifupi tu, asubuhi ya leo. Kwanza, ninataka kufanya kama nilivyoahidi kufanya, kuwaambia yale yote ambayo yametukia tu katika siku chache zilizopita, kuhusu kubadilika kwa huduma yangu. Halafu basi, ninalo somo fupi, kisha tuwaombee wagonjwa. Nami ninaamini kuna ubatizo, kwa sababu niliona dimbwi limejazwa.

18 Lakini kabla hatujaenda mbali zaidi, na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu sasa katika maombi. Nami ninashangaa, ni watu wangapi humu ndani ambao wanajua ya kwamba unamhitaji Mungu, na mngeinua mikono yenu kwa Mungu? Na kusema, mengi sana katika kufanya hivyo, "Unikumbuke, Bwana. Nina haja ya vitu hivi na vile."

Na tuombe.

19 Ee Bwana, kwa utulivu, tunatambua ya kwamba hatuna budi kuja kwa utulivu Mbele za Mungu. "Kwa maana mtu amjiaye Mungu lazima aamini ya kwamba Yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii." Nasi tunakuja katika utulivu wa Roho, kwenye Kiti Chako cha Enzi, Ee Mungu. Nasi tunainua mioyo yetu mbele Zako, na kusema, "Ichunguze, Ee Bwana." Na kukiweko na kitu chochote kichafu ndani yetu, kiondoe, Bwana, kama Mashariki ilivyo mbali na Magharibi. Na kukiweko na uovu wowote mioyoni mwetu, kitu ambacho kingeyazuia maombi yetu yasijibiwe, tunaomba ya kwamba Wewe utairuhusu Damu ya Bwana Yesu iondoe kila doa kutoka kwenye roho yetu na moyo wetu. Kwa kuwa imeandikwa, "Kama nikificha uovu moyoni mwangu, Bwana hatanisikia." Nawe uliiona hiyo mikono wakati ikiinuliwa, ambayo, kwa macho yetu ya kimwili, iliwakilisha haja ya mioyo yao. Tunaomba, Ee Bwana, ya kwamba Wewe utamjibu kila mmoja wao. Kuna wengi walio wahitaji.

20 Nasi tungeomba, katika kusanyiko la hawa watu asubuhi ya leo, ya kwamba utaukumbuka mkutano huu ujao wa San Jose. Tusaidie, Ee Bwana, wakati mamia ya maili ya theluji yako mbele zetu, kusafiri. Lakini tunaenda katika Jina la Bwana, kujaribu kufanya yote yaliyo ndani yetu, kuwasaidia watu Wako, Bwana, kuwasaidia waliopotea kukupata kama Mwokozi wao, na kuwasaidia walio dhaifu na vipofu, na kuinyorosha njia kwa ajili ya wengine watakaotufuata.

21 Libariki kanisa letu dogo na mchungaji wake, Ndugu yetu Neville, wadhamini wote, mashemasi, na walei, na walimu wote, na wote walioshirikishwa. Sio hao tu, bali makanisa yote yaliyowakilishwa hapa. Kwa hao vijana wanaume wanaoshikilia huko Sellersburg, tungeomba, Bwana, ya kwamba mkono Wako ungenyoshwa kwao, Bwana. Naomba uinue Kanisa lenye nguvu la Mungu aliye hai, huko Sellersburg. Tujalie, Bwana.

22 Waponye wagonjwa, wape vipofu kuona, watie nguvu wanyonge, na wokovu kwa wahitaji.

23 Tunapolisoma Neno Lako, asubuhi ya leo, jalia Roho Mtakatifu aje, aingie kwenye Neno na kulihuisha mioyoni mwetu.

24 Wabariki wale watakaobatizwa. Jalia wajazwe na Roho Mtakatifu, watakapotoka majini, wakimtukuza Mungu. Jipatie Mwenyewe utukufu, Bwana.

25 Na vile tumekusanyika, asubuhi ya leo, kwa ajili ya kutakaswa kwa nafsi zetu na mawazo yetu, jalia tuondoke kwenye maskani hii, asubuhi ya leo, tukiwa na azimio kubwa kuliko tulilowahi kuwa nalo, kukutumikia Wewe. Jalia tuishi, tumekusanyika pamoja, tumeshikanishwa na kuunganishwa na Roho Mtakatifu, mpaka siku ile tutakapokutana Nyumbani Mwako Utukufuni, kukizunguka Kiti Chako cha Enzi, ambako mamilioni watakuwa wakiimba, "Hosana! Hosana!" Jalia sote tuwe Huko, pasipo kukosekana hata mmoja. Tujalie, Bwana. Hadi wakati huo, tudumishe wenye afya, wenye furaha, na kujazwa na Roho wako, tukikutumikia Wewe. Mambo haya tunayaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

26 Bwana na aongeze baraka, tunaposoma sasa katika Kitabu cha Marko Mtakatifu, mlango wa 11, kuanzia kifungu cha kwanza. Ndipo basi baada tu ya nukuu hili dogo, ama maonyo, ndipo nitaingia kwenye somo letu. Hili ni somo kwa ajili ya yale ninayotaka kuwaambia.

*Basi walipofika*. . .

27 Samahani. Ninataka kuanzia kwenye kifungu cha 10, kuokoa wakati, kifungu cha 10 cha mlango wa 11.

> *Umebarikiwa na Ufalme ujao, wa baba yetu Daudi, unaokuja katika Jina la Bwana: Hosana juu mbinguni.*
>
> *Naye Yesu akaingia Yerusalemu hata ndani ya hekalu: na alipokwisha kutazama yote* pande zote, *kwa kuwa*. . .wakati wa jioni, basi *akatoka, akaenda Bethania pamoja na wale thenashara* wake.
>
> *Hata asubuhi yake walipotoka Bethania aliona njaa:*
>
> *Akaona kwa* mbali *mtini wenye majani, akaenda ili labda aone kitu juu yake: na alipoufikilia, hakuona kitu ila majani; maana si wakati wa tini bado.*
>
> . . .*Yesu akajibu akauambia, Tangu leo hata milele mtu* asile *matunda kwako. Wanafunzi wake wakasikia.*
>
> *Wakafika Yerusalemu: naye Yesu akaingia ndani ya hekalu, akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza na kununua ndani ya hekalu, akazipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao wauzao njiwa;*
>
> *Wala hakuacha mtu achukue chombo kati ya hekalu.*
>
> *Akafundisha, akasema,* Ime. . .*Je, haikuandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa*

*mataifa yote? Bali* nyinyi *mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi.*

*Wakuu wa makuhani na waandishi wakapata habari wakatafuta jinsi ya kumwangamiza: maana walimwogopa, kwa sababu...makutano wote walishangaa kwa mafundisho yake.*

*Na kulipokuwa* jioni *alitoka mjini.*

*Na asubuhi walipokuwa wakipita, waliuona ule mtini umenyauka toka shinani.*

*Petro akakumbuka habari yake, akamwambia, Rabi, tazama mtini ulioulaani umenyauka.*

*...Yesu akajibu, akawaambia, Mwaminini Mungu.*

*Maana amin, nawaambia, Yeyote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini; wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia; yatakuwa yake.*

*Kwa sababu hiyo nawaambia, Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*

28 Ni ahadi yenye neema jinsi gani! Na ni Kweli kabisa. Hili lilinishangaza, ama kama ninavyopaswa kutumia tamshi hilo, kwa muda mrefu. "Hilo lingewezekanaje?"

29 Basi wakati mmoja, wakati nilipoanza kuhubiri kwa mara ya kwanza hapa maskanini, miaka mingi iliyopita, nilikutana na neno la *kuzimu*. Ndipo nikafuatilia marejeo yake, mara nyingi, nalo likarejea kwenye *jehanamu,* katika Kiyunani, ambalo lilimaanisha, "kaburi." Wala sikujua la kusema, kwa sababu sitaki kuwajibikia nafsi za watu kwenye Siku ya Hukumu. Kwa hiyo nikalitafuta, na kutafuta, mpaka nikapata kilichokuwa Kweli. Kwa yapata miaka minne ama mitano, nisingeligusa somo la kuzimu, mpaka nilipopata Ukweli wake.

30 Ndipo basi Andiko hili likanishangaza, hata na zaidi, kwa sababu lilikuwa ni zuri sana, ahadi nzuri jinsi hiyo ikitolewa na si mwingine ila Yesu Kristo. Basi wakati alipowaambia wanafunzi Wake, "Mambo yoyote msemayo, yatakuwa yenu. Kama utauambia mlima huu, 'Ng'oka ukapelekwe baharini,' wala usione shaka moyoni mwako, lakini utaamini ya kwamba uliyosema yatatimia, yatakuwa yako." Loo, laiti tungaliweza kuyapima Maneno hayo! "Unaweza kupata yale *wewe* usemayo. Siyo yale Mimi nisemayo, bali yale uliyosema *wewe*. Utapata yale uliyosema."

31 Kwa miaka kadhaa, nilitulia juu ya hilo. Niliendea kila kamusi ya misamiati na fafanuzi, kila tafsiri, hata kwenye toleo la Douay. Na kila mfasiri analifasiri vile vile, "Unaweza kupata yale uliyosema." Kwa hiyo, ninajua ya kwamba, kama

limeandikwa katika Maandiko. Kwangu mimi, Maandiko yote ni Kweli. Na kama siwezi kulitumia kwa usahihi, lingali ni Kweli.

32 Kwa hiyo ninaamini, wakati mwingine, ya kwamba Mungu hutujalia kuona mambo kama wakati wetu wa kuyaona mambo umewadia. Yeye hushikilia baraka hizi. Kama vile baraka tunazofurahia siku hizi, babu zetu hawakuzifurahia hizo. Haukuwa ni msimu wake.

33 Ningeweza kukumbuka wakati Roho Mtakatifu . . . ule usiku niliporudi kwenye dawati lili hili, kutoka kwenye kile kinu, ambako nilikuwa nikiombea. Ndipo nikawaambia wengi wenu watu mnaoketi hapa, ya kwamba Yeye alikuwa ameniagiza, kwa Roho Wake, agizo kwa ulimwengu mzima, kwamba, "Viwete wangetembea, na vipofu wangeona, na wafalme na watawala wangekuwa wakipiga simu kwa ajili ya maombi. Nalo lingeanzisha uamsho miongoni mwa ndugu, ambao ungeenea kote ulimwenguni, kabla ya Kuja kwa Bwana."

34 Ilikuwa ni vigumu kuamini hilo. Ilikuwa ni vigumu kwangu kuliamini. Lakini hilo ndilo lililotukia. Limefanya tu jambo hilo. Mpaka, leo hii, mioto ya uamsho wa Roho Mtakatifitu inawaka, kote ulimwenguni: India, Afrika, Asia, kote katika Ulaya, na kila mahali. Watu wa Roho Mtakatifu, waliojazwa na Roho, wakiuwasha moto ulimwengu, kwa uamsho wa Nguvu za Kristo aliyefufuka; viwete watembea, vipofu wanaona, viziwi wanasikia, bubu wanaongea. Kila namna ya miujiza ya ajabu inaendelea, kwa sababu Mungu aliliahidi. Nayo ahadi ya Mungu ni ya kweli.

35 Basi ninapoanza kuwazia juu ya jambo hili, nisingeweza ila kumuuliza Yule aliyekuwa akisema nami, "Nilikuwa sifai." Nadhani ilimbidi Mungu kumchukua maskini mtu mdogo, asiyejali, asiye na elimu, kwa sababu, katika jambo hili, Yeye, Mungu, huchukua kitu ambacho ni duni, kitu ambacho kimetupwa nje.

36 Hilo ndilo linalonifanya kuwapenda watu wa Mungu hivyo. Wanawatupa nje, kama "watakatifu wanaojibingirisha, ama watu haramu." Lakini hapo ndipo Mungu yuko tayari kuwachukua na kufanya jambo fulani nao. Nalo linampendeza. Hilo linaonyesha ya kwamba Yeye ni Mungu, huchukua kitu duni na kufanya kitu kutoka kwake. Anamchukua mwenye dhambi kama mimi, na kumfanya Mkristo; mkono wa Mungu.

37 Nilimwuliza juu ya huo uwezo. Naye akaniambia ya kwamba nitawaombea wagonjwa. Nalo hilo agizo lilikuwa, "Wafanye watu kuamini na uwe mwaminifu, ndipo hakuna kitu kitakachosimama karibu na hayo maombi." Wengi wenu hapa mnakumbuka hilo. Limeandikwa kwenye vitabu, kote ulimwenguni.

38 Niliuliza, "Ningewezaje kufanya jambo hilo wakati sikuwa na elimu?"

39 Akasema, “Kutakuwa na ishara mbili utakazopewa, kama alizopewa Musa. Na moja ya hizo ingekuwa karibu, kama vile mkono wa Musa, Yeye aliugeuza kutoka ukoma ukapona.” Ndipo—ndipo basi jambo lilo hilo likatukia, kuhusu kuuweka mkono wangu juu ya watu, na halafu jinsi ambavyo hilo lilijidhihirisha. Kisha akasema, “Utajua siri zenyewe za moyo wao.”

Na mimi—mimi nikasema, “Hiyo ndiyo sababu niko hapa.”

40 Akasema, basi, akanielezea Maandiko. Na, loo, tangu wakati huo, Biblia imekuwa Neno jipya kwangu. Nilikuwa na mtazamo tofauti juu Yake, mtazamo tofauti Wake. Jambo fulani lilitukia.

41 Halafu, baadaye kidogo, akasema, “Ndipo kama utakuwa mwaminifu, ukae mnyenyekevu, ujiepushe na pesa na kadhalika,” kasema, “basi itaendelea tu kukubariki, nawe utaendelea kupanda.”

42 Ni mara ngapi tunapowaangalia watu wanaopanda juu katika wadhifa mkuu, kitu kama hicho, na kupata majina makubwa, lakini wakati mwingine hicho sicho Mungu anachokiita kikuu.

43 Mnakumbuka wakati Yohana, wakati alipokuja akihubiri? Biblia ilitabiri, ya kwamba, “Kila mlima utashushwa, na kila bonde litainuliwa.” Mnaona? Ndipo wakati alipokuja, mngewazia atashuka kutoka Mbinguni pamoja na magari farasi ya moto. Lakini ilikuwa ni nini ila maskini mtu aliyejifunika kipande cha ngozi ya kondoo, na huko nje ufukoni mwa Yordani, akihubiri. Kwenye ufuko uliojaa matope, si hata kanisani, bali Mungu aliita hilo “kuu.”

44 Ndipo Yesu alipowaambia wanafunzi, ya kwamba, “Hapakuwapo na mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama Yohana Mbatizaji.” Hebu wachukue wafalme wote, na Daudi, nabii, na fahari Yake yote kuu katika Sulemani, hata hawakumgusa Yohana. Na, hata hivyo, hata hakuwa na mahali pa kulaza kichwa chake.

45 Kwa hiyo, haikubidi kuwa tajiri na mwenye nguvu katika ulimwengu huu, upate kuwa mkuu machoni pa Mungu. Inakubidi tu kuwa mnyenyekevu moyoni mwako. Naye Mungu anaita hilo “ukuu,” yeye aliye mkuu vya kutosha kujinyenyekeza. Huyo ni mtu mkuu, ambaye—ambaye atachukua lawama ya kila kitu, atakayejinyenyekeza. Huo ndio ukuu.

46 Kisha tunaona ya kwamba, hili ndilo Mungu alilosema. Kisha likatamkwa kutoka mimbarani hapa, mara ya kwanza. Lilifanya jinsi hasa lilivyosema litafanya. Likatokea kanisa la Kipentekoste, likashika uamsho. Na, siku hizi, kanisa la Kipentekoste ndilo kanisa linalopanuka upesi sana kote ulimwenguni. Mwaka jana walisajili . . . Hiyo haitujumuishi sisi na—na hawa walio nje ya madhehebu . . . Waongofu milioni moja

na laki tano, mwaka jana, ambayo iliwahusisha Waprotestanti wengine wote, wakiwekwa pamoja, na Ukatoliki, pia. Ukatoliki ulikuwa tu na, naamini, mia nne na sabini na tano elfu, kitu kama hicho, waongofu, kote ulimwenguni. Lakini Pentekoste ilifikia milioni moja na mia tano elfu. Mungu analitayarisha Kanisa Lake.

47 Watu wasio na elimu, wa hadhi ya chini, wakiinuka katika Nguvu za upako wa Roho, wakitoka pasipo elimu yoyote wala chochote kile, na kuutangaza utajiri wa Kristo usiotafutika. Hicho ndicho kikuu machoni pa Mungu.

48 Nasi tunaona, basi, kwamba mambo haya yote yaliuwasha moto, naye Roho Mtakatifu akawa mwaminifu kwa Neno Lake.

49 Baada ya yapata miaka mitano ya kuwashika watu kwa mkono, basi usiku mmoja, katika Queen's City, huko Regina, huko Canada, mtu mmoja alipitia kati ya jukwaa, na hapo maisha yake yakafichuliwa dhahiri tu yalivyoweza kuwa, mbele ya Roho. Palikuwapo na upambanuzi, kama Yeye alivyoahidi. Hilo limekuwa kote ulimwenguni. Limechapishwa katika lugha nyingi, nyingi sana karibu kote ulimwenguni, mpaka ulimwengu wote unajua habari zake. Ndipo adui akaingia na kulidhihaki, na kusema, "Ilikuwa ni kusoma akili." Kisha kulikuwako na maigo yake, na kila kitu kingine. Lakini katikati ya hayo yote, Mungu aliendelea moja kwa moja, vivyo hivyo. Mungu alidumu mwaminifu kwa ahadi Yake aminifu. Atafanya hivyo, kila wakati.

50 Sasa tunaona, baadaye, basi, siku moja nilikuwa nikienda ku—kuvua samaki, huko chini Dale Hollow, pamoja na watu fulani, Bw. Wood na ndugu yake. Nao walikuwa ni Mashahidi wa Yehova, na walikuwa ndio kwanza waongoke na kubatizwa katika Imani. Basi tulipokuwa tukivua samaki, karibu na ufukoni... Nimewasimulia hadithi hiyo, mara nyingi. Hapo Bw. Wood akasema, yule Banks Wood, ambaye, mmoja wa wadhamini wetu hapa sasa, akasema kuhusu dada fulani mkongwe aliyekuwa akiwalisha kipande cha mkate wa kuokewa nyumbani pamoja na siagi. Alikuwa ni mfuasi wa Church of God. Ndipo kasema, "Lyle," kwa ndugu yake, "inatupasa kukwea kule na kumwambia tuliokoka."

51 Mwajua, kuna mambo fulani tu tunayoweza kusema, yanayoshikamana na Roho Mtakatifu. Mambo fulani tu yanayompendeza vizuri tu, na tunaposema jambo hilo. Ninawatakeni muone, "Yale usemayo." Laiti tungaliweza kupata tu la kusema! Maneno yako hukuhukumu. Maneno yako hukuhukumu, ama maneno yako yatakubariki.

52 Na, bila kujua, hapana shaka Banks alisema jambo lifaalo. Kwa kuwa mara aliposema hivyo...

53 Nilikuwa nimeketi nyuma ya mtumbwi, nikivua samaki kwa ndoana, samaki mdogo wa shavubluu; wa kuwekwa kwenye

ndoana, kama chambo, kwa kuwa tulikuwa tumeishiwa na chambo. Nami nilikuwa nikiwashika samaki hawa wadogo na kuwaweka kwenye ndoo, kwa ajili ya ndoana kubwa.

54 Basi Banks aliposema hivyo, mara Kitu Fulani kikanigusa. Yeye alisema jambo lifaalo. Ndipo Roho Mtakatifu akanena na kusema, "BWANA ASEMA HIVI. Mtapata, katika saa chache zijazo, kutakuwako na ufufuo wa mnyama mdogo." Nilifikiri ingekuwa ni mtoto wa paka ambaye niliwazia mvulana wangu alikuwa amemfinya kwa nguvu kupita kiasi, na kuiminya pumzi kutoka kwake, na—na alikuwa amemwangusha sakafuni, kabla hatujaondoka. Nilidhani angekuwa ni huyo. Lakini tulishangaa, kesho yake asubuhi, tulipokuwa tumeketi kwenye huo mtumbwi . . .

55 Ninajua Banks yuko hapa. Nadhani Lyle . . . Lyle yuko hapa, Banks? Ama, kama upo, Lyle, inua mkono wako. Yeye hushuka, yuko pamoja nasi, wakati wote.

56 Yeye alikuwa . . . alishika samaki, kwa moja . . . ndoana ndefu. Naye akamshika samaki wa shavubluu, naye akaimeza hiyo ndoana ndani kabisa. Ndipo akamshika maskini samaki huyo. Badala ya kuitoa tu hiyo ndoana kutoka kinywani mwake, ilikuwa imeshika ndani sana, mpaka, yeye aliivuta tu. Basi akalivuta tu—tumbo, na matumbo, na mashavu, na kila kitu, moja kwa moja kutoka kinywani mwake. Naye akamtupa tu huko majini, maskini samaki mdogo tu kama tuliokuwa tukitega samaki nao, usiku uliotangulia, nasi tulikuwa tumekatakata mia moja wa hao, ama zaidi, tupate chambo. Basi maskini jamaa huyo akatetemeka mara nne ama tano, na kujaribu kupanua maskini kinywa chake, bali asingeweza, kwa kuwa alikuwa amejaa mashavu na kadhalika. Naye Lyle akasema, "Umepumua ya mwisho, maskini jamaa mdogo." Nikaendelea, kuvua samaki, pasipo kuwazia lolote juu yake.

57 Basi, Mungu hufanya mambo kiajabu sana. Mara, nikahisi pale kitu Fulani kikija, kikishuka chini juu ya miti. Roho Mtakatifu akashuka chini na kusema, "Simama." Kasema, "Nena na huyo samaki mdogo, naye ataishi tena." Alikuwa amelala pale, amekufa, kwa nusu saa, tayari ameelea akarudi kwenye magugu.

58 Nikasema, "Samaki mdogo, ninakupa uhai wako, katika Jina la Bwana Yesu." Maskini samaki huyo mdogo akapinduka, akageuka upesi akaenda kupitia majini upesi alivyoweza. Nikasimama pale, pasipo kujua la kufanya.

Ndugu Banks Wood akasema, "Ni vema kwetu kuwa hapa."

59 Naye Lyle akasema, "Hiyo ilimaanisha mimi, kwa sababu nilimwambia jambo hilo, 'Ulipumua kwa mara ya mwisho, jamaa mdogo.'" Naye akasisimkwa sana.

60 Nikasema, "La, sivyo." Nilikuwa nikijaribu kumfariji Lyle. Nikasema, "Sivyo ilivyo."

Ndipo Andiko hili likanijia tena.

61 Nilikuwa na angalau watoto mia moja wenye kifafa kwenye orodha, wa kuombea, watu wengi wenye lukemia na kansa, na kifua kikuu, wakiliwa, vipofu, na viziwi, na bubu. Kuna ukurasa baada ya ukurasa, nyumbani kwangu, uliojaa hao, na inaonekana kana kwamba Mungu mwenye rehema angewajalia hao badala ya kuzitumia Nguvu Zake juu ya maskini samaki mdogo, asiye na maana.

62 Lakini Yeye anadumu Mungu. Kwa nini hakutumia Nguvu Zake juu ya wenye ukoma langoni, badala ya maskini ule mtini? Hilo ni la kufanya nini? Mungu anataka kuonyesha ya kwamba anajali. Yeye anajua mambo yote. Yeye ni Mungu, juu ya mtini. Yeye ni Mungu, juu ya samaki. Yeye ni Mungu, juu ya maumbile. Yeye ni Mungu, juu ya vitu vyote, wala hakuna kitu kilicho kidogo kupita kiasi ama kisicho na maana asichokijali. Kwa hiyo hilo lingetujalia kujua, ingawa sisi ni wadogo na wasio na maana, Mungu anapendezwa na sisi kumfanyia jambo fulani. Yeye anapenda kuonyesha Utukufu Wake.

63 Basi hilo lilinishika kwa nguvu sana, hata nisingeweza kupumzika, mchana na usiku. Hiyo imekuwa miaka miwili iliyopita, na daima imenisumbua. Nami ningesema, "Loo, kamwe siwezi kusema lolote kulihusu, kwa kuwa siwezi kuliweka kwenye ule Upatanisho. 'Lolote *wewe* usemalo, litatimia. Waweza kupata lile *wewe* usemalo.'" Nami nimesimama hapa kwenye mimbara ii hii, na kujaribu, na kuyaendea Maandiko; na kuyaacha, na kurejea nyuma, kwa sababu niliogopa kuyatumia. Huwezi kuwa na imani isipokuwa unajua kile unachofanya.

64 Jamaa fulani alinijia, sio muda mrefu uliopita, na akasema, "Ndugu Branham, unafikiri ni vibaya kwa Mkristo kuvuta sigara?"

65 Nami nikasema, "Kwa nini kuniuliza?" Iwapo kuna swali niani mwako, liache. Kamwe usininii . . .

66 Huwezi kuwa na imani isipokuwa una hakika kabisa kwamba uko sahihi. Wakati vivuli vyote vimetoweka, basi unaweza kuwa na imani na matumaini.

67 Wala nisingeweza kwenda kule nje na kulihubiri Andiko hilo, bila kujua yale niliyokuwa nikizungumzia. Lakini, hata hivyo, nilijua lilikuwa ni la Bwana. Wengi wenu nyinyi watu mnanishuhudia, ya kwamba, kwa miaka miwili iliyopita, sikuzote mmenisikia, kutoka kwenye jukwaa hili, nikisema kwamba kuna kitu fulani, kitu fulani, mahali fulani. Ninakifikia. Ninajua kiko karibu sana. Kamwe inaonekana siwezi kukishika. Nitasema, "Ninalifikia Andiko pale, sijui la kufanya."

68 Kwa sababu, Maandiko, loo, huenda ukaweka tafsiri. Kama mtu fulani angaliniuliza, ningaliwaambia jambo fulani, na

kuondoka, na kuliweka kwenye kitu kingine. Bali kukabiliana na hiyo hoja . . . Ni kama tu, hatuna budi kukabiliana na ile hoja, je, ubatizo wa Roho Mtakatifu ni wa kweli ama ni wa uongo? Inatubidi kukabiliana na ile hoja, je, Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Hiyo ni kweli ama ni uongo? Hatuna budi kukabiliana nalo. Hatuna budi kujua ya kwamba Neno la Mungu daima ni kweli.

69 Kwa hiyo, likaendelea mbele, na huku na huku. Nami ningeliweka niani mwangu, wala kamwe nisingeweza kuliondoa. Na kila mahali ningeenda, daima lingenijia, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka ukatupwe baharini,' wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako."

70 Nikawazia, "Inawezekanaje, Bwana? Hiyo ingekuwa ni *mimi* nikilisema. Ningeninii . . . Lisingefaa kitu, kwa kuwa ingekuwa ni *mimi* nikilisema. Kwa hiyo, siwezi kusema chochote ila kile Wewe ulichosema. Na mimi—mimi ninasema tu hilo, kwa Maandiko."

71 Basi vitu vyote vilitulia juu ya Upatanisho. Hakuna baraka nje ya Upatanisho. Maana, sisi ni wenye dhambi, nje ya Upatanisho. Kama lingalikuwa tu ni jambo la ulimwengu mzima kwa ajili ya kila mtu, basi kila mtu angeokolewa. Lakini ni msimamo wako juu ya baraka za Upatanisho, ndio unaokuletea hizo baraka.

72 Kama vile wokovu, kulingana na Mungu, niliokolewa wakati Yesu alipokufa. Bali hautanifaa kitu mpaka ifunuliwe kwangu ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, nami nimemkubali kama Mwokozi wangu. Na kila Andiko ni vile vile.

73 Uponyaji wa kiungu ni kwa ajili yako, kama Mungu atakufunulia huo, ya kwamba huo ni kwa ajili yako. Lakini huwezi kuupata tu kwa bahati. Hauna budi kuja kwa ufunuo. Basi unapofunuliwa, ya kwamba, "Kwa mapigo yake wewe uliponywa," hakuna kitu hata Shetani anachoweza kufanya.

74 Kama vile ndugu yetu mdogo kutoka Sellersburg alivyosema, "Ibilisi wote wasingeweza kulitikisa," hakika, wakati jambo fulani limefunuliwa.

75 Angalieni. Basi, katika msimu huu wa kupukutika uliopita, wengi wameniambia, "Ni kwa nini, kila asubuhi, wewe, unapokuwa nyumbani, unanyakua bunduki yako na kuelekea mwituni kuwinda?"

76 Ninawatakeni mjue ya kwamba Yeye ni Mungu wa msituni kadiri tu alivyo Mungu wa mjini. Yeye ni Mungu huko nje kadiri tu alivyo hapa. Naye Mungu sikuzote huwashughulikia watu kulingana na uwezo wao, na chochote. Kama vile Daudi, karibu na maji matulivu na majani mabichi, kwa sababu alikuwa ni mchungaji. Na njia mbalimbali alizo nazo, kufunua, na jambo fulani.

77 Ningeamka, asubuhi, kwenda mwituni, mapema sana, yapata saa kumi, kuwinda kuchakulo. Naye mke wangu hata aliniambia, alisema, "Billy, hivi huchoki kwenda kuwinda?" Mnaona, unavishinda vita hivi, peke yako. Mke wangu halielewi. Silielewi mimi. Lakini ni vita. Inakubidi kusimama, peke yako. Hakuna mtu anayeweza kusimama pamoja nawe. Ipo nafasi tu kwa ajili yako na Yesu. Ati kufahamika vibaya? Hakika.

78 Hata kwa msichana wangu mdogo pale, Rebekah. Kasema, "Kama nikipata kuolewa na mwanamume, kama hata akitaja kwenda kuwinda, hatanioa." Kasema, "Najua yale mama yangu amepitia. Mume ametoka, na ameenda mikutanoni; mara anapokuja nyumbani, ananyakua maskini bunduki ama ufito wa kuvua samaki, na kuingia mwituni."

79 Nikasema, "Ungetaka yeye angalau afanye hivyo, ama unaona afadhali angenyakua jozi ya karata ama—ama mwenye nywele za rangi ya manjano fulani, na kuondoka? Sasa chukua tu maoni yako."

80 Niliporudi siku hiyo, yeye alisema, "Baba, naomba msamaha kwa hilo. Nitaolewa na mtu kama wewe, anayependa kuwinda, halafu nitaenda kuwinda pamoja naye." Akasema, "Nitaenda huko nje pamoja naye."

81 Nikasema, "Vema, hilo ni sawa, pia. Laiti ungalizungumza na mama yako kidogo, juu yake."

82 Lakini ni kitu fulani huko msituni. Wakati nilipomjua Mungu kwa mara ya kwanza, nilitaka kutubu. Sikujua jinsi ya kutubu. Sikujua jinsi ya kuzungumza na Yeye. Kwa hiyo, nikaketi chini, na kumwandikia barua, na kumwomba anisamehe. Wala sikujua jinsi ya kufanya hivyo. Kwa hiyo nilijua ya kwamba nilikuwa nimehisi kitu fulani, huko msituni, nami nikaitundika mtini, ili akishuka kupitia msituni, katika mahali nilipokuwa nimemwona Yeye, kwamba angeweza kuisoma hii, na angeelewa niliyomaanisha, kwamba nilisikitika sikuwa nimemtumikia, nami ninataka anisamehe dhambi yangu.

83 Ndipo nikajionea aibu, na kuichukua. Nikasema, "Kama yeye ni Mwanadamu, ataelewa kama mwanadamu. Yeye ni Muumba wangu." Ndipo nikapiga magoti kibandani na kuanza kumzungumzia kama mwanadamu, na Yeye akanijibu kama mwanadamu. Basi ilikuwa kwenye . . .

84 Ninazo tarehe zilizowekwa hapa chini. Tarehe 12 Oktoba . . . Tarehe 15, msimu wa paa ulikuwa unaanza, huko Wyoming. Tarehe 12 ilikuwa ndiyo siku ya mwisho ningeweza kuwinda, nasi tulikuwa tuondoke tarehe 12. Ninamaanisha, tarehe 10 tulikuwa msituni, ambayo ilikuwa ni Jumamosi. Jumapili, nilihubiri, ambayo ilikuwa ni tarehe 11. Jumatatu, Ndugu Sothmann na Ndugu Roberson huko nyuma, na sisi sote, tuliondoka kwa—kwa ajili ya mkutano, ama kuwinda paa huko Wyoming. Asubuhi hiyo, ya tarehe 10 ambayo

ingekuwa . . . Halafu, tarehe 18, huo msimu ungefungwa Indiana, tusingewinda kuchakulo tena.

85 Kwa hiyo nikasema, "Huu utakuwa ndio wakati wa mwisho ninaoweza kwenda nje." Basi tukakusanya kundi moja pamoja, nami nikawatawanya msituni. Nikarudi, huko juu mahali ambapo ninapenda kwenda, huko Salem. Msimu ulikuwa umechelewa. Kuchakulo walikuwa ni wachache. Nilikuwa nimetoka mara kadhaa, nikimpata tu kuchakulo mmoja kwa wakati mmoja.

86 Kwa hiyo, asubuhi hii, nikaingia kwenye msitu ule ule, ndipo upepo ukainuka na kuanza kuvuma. Basi mtu yeyote ambaye huwinda, anajua hiyo ni asubuhi mbaya. Nikawinda kote msituni, pasipo kuona kuchakulo mmoja, wala kumsikia mmoja. Nikashuka chini kabisa ya kijito, kisha nikaanza kupanda nipate eneo jingine dogo la msitu. Basi nilipokaribia kichaka hiki kidogo, kulikuwako na mi—mijozi mingi, na miti ya nzige, majani yote yamepukutika, kichaka tu kitupu. Karibu nayo, mikuyu miwili. Sasa, kuchakulo hawakai karibu na mikuyu. Lakini papo hapo juu kutoka kwake, niliona, ilionekana kama, nilipata mtazamo wa haraka . . . Nilipata mtazamo wa mara moja wa kuchakulo akipitia msituni, ila alikuwa akikimbia upesi.

87 "Loo," nikasema, "hakuna haja ya kuwinda. Hawa hapa watu hapa nje, wakulima wakivuna mahindi yao, papa hapa karibu na kichaka hiki kidogo. Kuchakulo hawatakuwa hapa." Kwa hiyo nikaketi chini kati ya hiyo miti miwili, na kutegemeza miguu yangu juu ya mmoja na kuegemea kwenye huo mwingine, katika jua lenye joto. Nikawazia, "Nitalala kidogo tu, kisha nitawachukua Ndugu Banks, na Ndugu Sothmann, na hao wavulana, wakati nikirudi, na chini barabarani.

88 Basi nikiketi pale . . . [Ndugu Branham anakohoa mara mbili—Mh.] (Samahani.) Nilipoketi pale, chini ya huo mti, niliiridhisha tu nafsi, huku jua lenye joto linaniangazia. Kitu Fulani kikasema, "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka ukatupwe baharini,' wala usione shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba mambo hayo ambayo umesema yatatimia, unaweza kupata yale wewe uliyosema."

89 Nikasema, "Vema, sasa, hilo hapo lile Andiko niani mwangu tena." Nikasema, "Nina wakati mdogo hapa, yapata saa moja kabla haijanibidi kwenda kuwachukua hao wavulana wengine, kwa hiyo nitayasoma tu Maandiko hayo." Kisha nikasema, "Sasa, hilo lingetumikaje?" Kasema, "Hii hapa njia pekee lingaliweza kuwa, kwamba, hao wanafunzi waliishi ng'ambo ya pili ya ule Upatanisho. Upatanisho ulikuwa ni baadaye, yapata, loo, majuma kadhaa baadaye, kabla ya Upatanisho kufanywa. Yesu aliwapa Nguvu, upande ule mwingine wa Upatanisho, kama alivyowafanyia wale manabii."

90 Basi niliposema, “manabii,” kitu Fulani kikanigusa tena. “Manabii walikuwa nini?” Ndipo nikaanza kuwazia, kuhusu yale aliyofanya na manabii.

91 Nalo likafikia, baada ya kuwa nikizungumza pale kwa kitambo kidogo, ndani yangu, nikiwazia tu, mpaka nikatambua dhahiri kitu Fulani kilikuwa karibu, hata nikawa ninazungumza na mtu Fulani. Basi kitu Fulani kikaniambia, “Hilo liko katika Upatanisho. Kwa kuwa kama mwanamume ama mwanamke akijiweka wakfu sana na kujitolea kwa Mungu, hata Mungu aingie tu ndani na kuitumia sauti yao, basi si huyo mtu anayenena. Ni Mungu aliye ndani yake anayenena.”

Nikawazia, “Hiyo ni kweli.”

92 Kitu Fulani kikaniambia, “Unafikiri ni nani . . . Unaonaje maono hayo jukwaani? Unaonaje maono hayo hapa nje? Ni kitu gani? Unafikiri ni hekima yako mwenyewe kwamba ungeweza kutabiri jambo fulani ambalo lingetukia kila wakati kikamilifu? Unafikiri ni wewe unayenena? Ungewazia wakati mwingine . . . Wakati Roho Mtakatifu anapoingia katika Ujumbe, wala hujui la kusema, ni kitu gani kinachonena wakati huo? Ni kitu gani wakati mtu atanena kwa lugha asiyojua neno kuihusu? Ni kitu gani kitakachofasiri lugha iyo hiyo, huku hakuna hata mmoja wao anayejua lolote kuihusu? Ni huyo mtu binafsi, ama ni Roho wa Mungu aliye hai?”

93 Nikasema, “Hiyo ni kweli. Ninaliona. Ni Mungu anayenena. Na yote kanisa linayohitaji ni hatua moja karibu zaidi Naye, maisha yaliyowekwa wakfu zaidi, kuishi pamoja Naye.”

94 Basi nilipokuwa nimeketi pale, kwa dakika moja tu ama mbili, nikiliwazia jambo hili, nilijikuta nikizungumza na mtu Fulani. Ndipo nikasikia kitu Fulani kikisema, “Omba. Sema utakalo, nalo litatimia.”

95 Nikasema, “U nani Wewe?” Nikasema, “Kwani ninazungumza na nani? U nani Wewe? Ni nani anayesimama hapa katika vichaka hivi, ambapo ninaweza kuisikia Sauti hiyo ikisema nami? U nani Wewe? Sema nami.” Nikasisimkwa sana na kuruka juu kutoka katikati ya miti hiyo. Nikasema, “Sema nami. U nani Wewe? Siwezi kukuona.” Nikaitafuta Nuru hiyo pale. Nisingeweza kuona chochote. Nikasema kwa sauti kuu, “U nani Wewe? Uko wapi? Unataka nini nami? Bwana, uko wapi?”

96 Kitu Fulani kikarudi nyuma, na kusema, “Sema utakalo nawe utapewa.”

97 Nikasema, “Bwana, hivi unaibadilisha huduma yangu? Hili ndilo badiliko ambalo umekuwa ukizungumza habari zake? Hiki ndicho inachokujia? Hivi ndivyo itakavyokuwa? Kitu fulani katika ile nyumba ndogo niliyoona katika ono, ndicho hiki?”

98 Mara upako mtamu sana wenye kilindi wa Roho Mtakatifu ukaniinua, hivyo, kutoka kwa miguu yangu, na kusema, “Sema utakalo, nawe utapewa.”

99 Nikasimama hapo, nimeduwaa. Ukaniacha. Sikuwa na chochote. Nikawazia, “Vema, niseme nini? Hakuna wagonjwa hapa. Hakuna kitu hapa. Niko msituni. Niseme nini? Ni—ni—nifanye nini?” Nami nikawazia, “Kwani ninaingia wazimu? Kwani nimesoma kwa bidii sana hata nguvu zangu za kiakili zinavurugika?”

100 Ndipo papo hapo nikaisikia tena, kama tu vile mnavyonisikia, kasema, “Wewe si unawinda, wala huna mnyama?” Kasema, “Nena chochote utakacho.”

101 Vema, nikawazia hili, “Mungu alisema, ‘Thibitisha mambo yote.’” Nikasema, “Bwana Mungu, ikiwa huyo ni Wewe, na hii ni ishara kwamba uko karibu kubadilisha huduma yangu kutoka kwenye maono hayo, iwe kitu kikuu zaidi, ambacho nimekitazamia muda mrefu sana,” nikasema, “jalia iwe kwamba utayajibu maombi yangu.” Ndipo nikasimama hapo kidogo. Nami nikawazia, “Alisema nini? Hakusema, ‘Omba.’ Alisema, ‘Sema utakalo. Liseme tu, nayo maneno yako yatatimia. Uambie mlima huu, nao utafanya tu yale uliyosema.’”

102 Kwa hiyo nikaliegemeza bega langu kwenye mti. Nami nimezoea. . . Nimeikarabati bunduki yangu kwenye yadi hamsini, kupiga shabaha. Kwa hiyo ni—nikaangalia pande zote, kuona mti ulio umbali wa yadi hamsini. Nao ule uliokuwa umbali wa yadi hamsini, hauna—hauna majani. Nikasema, “Karibu haiwezekani kabisa kwa kuchakulo kuja kwenye mti ule, papa hapa, huku wale wakulima pale wanavuna mahindi yao.” Nikasema, “Lakini kutakuwako na kuchakulo mwekundu huko mwisho wa lile tawi na kuketi pale chini, nami nitampiga risasi kutoka hapa.”

103 Mara niliposema hilo, huyo hapo kuchakulo. Nikatetemeka kidogo, nikamlenga, na kumpiga risasi huyo kuchakulo. Nikaenda pale na kumwokota. Nilikuwa ninatetemeka, mwili mzima.

104 Nikasema, “Labda hilo lilitukia tu namna hiyo.” Mnajua jinsi watu wanavyoweza kutilia shaka. Lakini unataka kuwa na hakika. Usifanye lolote isipokuwa una hakika kabisa, ndipo unajua yale unayofanya. Nikasugua uso wangu kidogo, nikaangalia, risasi ya jicho kikamilifu. Kwa hiyo nikaenda na kuketi chini kando ya kilima, ndipo nikasema, “Bwana, imeandikwa katika Neno Lako, ya kwamba, ‘Kinywa cha mashahidi wawili au watatu, kila neno na lithibitike.’” Nikasema, “Kama huyo alikuwa ni Wewe, nisamehe ujinga wangu. Ila nakuomba unipe kuchakulo mwingine kama huyo, na,” nikasema, “ndipo nitakuamini, kwamba ni Wewe, wala

ibilisi hatakuwa na nafasi yoyote ya kusema ya kwamba lilitukia tu jinsi hiyo." Kwa hiyo nikaketi chini.

105 Kwa dakika moja tu, huu hapa Huo unakuja, ninauita, "Upako mkuu," ukaingia tena. Nami karibu niinuliwe juu. "Basi sema, sema utakalo, nawe utapewa."

106 Nikaangalia kote msituni mpaka nikaupata mti mwingine umbali wa yadi hamsini, uliokuwa na vichaka vingi ndani yake, na mizabibu na kadhalika imejizungushia kote, ambapo ni nadra sana kuchakulo kupanda mti kama huo. Nikasema, "Na kutakuwako na kuchakulo mbweha mwingine mdogo ameketi pale pale." Ndipo nikashusha kidole changu, na kuangalia kote kwenye huo msitu.

107 Kisha nikaangalia nyuma, naye kuchakulo mbweha aliketi pale akiniangalia moja kwa moja, tena. Nikampiga huyo risasi. Nikamwokota. Ndipo nikawazia . . . Loo, nilikuwa nikitetemeka.

108 Nikawazia, "Wazia! Mungu mkuu wa Mbinguni yuko hapa mwituni, na Yeye ananithibitishia, kwa njia yangu mwenyewe, nikiwinda hapa, ya kwamba Yeye atafanya vile hasa alivyoniambia miaka kumi na mitano iliyopita." Nikaangalia kidogo. Nikasema, "Bwana, litatukia tena."

Akasema, "Sema mahali atakapokuwa."

109 Nikasema, "Nitalifanya hili gumu." Nikasema, "Kile kisiki cha kale kilichojificha kilichochomoza huko nje, kando ya lile shamba, kitupu, laini na cheupe." Nikasema, "Kutatokea kuchakulo mwingine mwekundu, naye ataenda kwenye ncha ya kisiki kile, na kuangalia shambani, kwenye wale wakulima. Hiyo itakuwa ni hivyo."

110 Nikaangalia nyuma wala hapakuwapo na kuchakulo yeyote pale. Nikaangalia kwa yapata dakika tano. Bado hapakuwapo na kuchakulo. Ni—nikasema, "Vema," nikasema, "wawili, kuchakulo wawili ni sawa." Nikasema, "Wawili ni shahidi. Nitaliamini hivyo."

111 Ndipo kitu Fulani kikasema, "Lakini ulisema kungekuwako na mmoja." Nikangojea dakika zingine tano. Hakuna kitu. Nalo likaendelea kurudia moyoni mwangu, "Ulisema kutakuwako na mmoja." Nikangojea na kungojea. Kitu Fulani kikasema, "Kwani unaona shaka?"

Nikasema, "Hata."

112 Na mara niliposema hivyo, kutoka kwenye tawi hilo akatokea kuchakulo mwekundu, akasimama na kuwaangalia wale wakulima. Mungu ndiye hakimu wangu, nikisimama hapa. Nikampiga huyo kuchakulo risasi, nikaenda na kumwokota. Nami nikatembea mwituni mpaka nikawa nimechelewa saa nyingi sana kwenda kuwachukua wale wavulana, kuona kama kungekuwako hata na mwingine mmoja, mahali popote. Wala hapakuwapo.

Ndipo nikaja nyumbani, nikawasimulia yote.

113 Halafu basi tarehe 7 Novemba, nilikuwa huko chini Kentucky. Nilikuwa pamoja na shemeji wa Ndugu Wood, anayesimama pale, Charlie Cox, anayesimama pale kwenye nguzo chomozi. Na pamoja na Ndugu Tony Zabel, mmoja wa mashemasi hapa kanisani. Uko hapa, Tony? Yuko hapa mahali fulani, Ndugu Tony Zabel, na pia Ndugu Banks Wood. Nasi tulikuwa juu milimani, tukiwinda. Ndipo nikaelekea mwituni, nao kuchakulo walipatikana kwa shida sana. La . . . Majani yameingia kilindi, ardhini. Ndipo nikaelekea msituni.

114 Ndipo kitu Fulani kikaniambia, "Unataka kuchakulo wangapi asubuhi hii?"

115 Nikasema, "Vema, nimepata mia moja na kumi na wanne mwaka huu, ama mia moja na kumi na saba." Nikasema, "Kama ningalipata watatu zaidi, ingewafanya mia moja na ishirini. Hiyo ingefanya namba shufwa ya kumalizia." Nikasema, "Jambo lingine ingekuwa, ingenipa sita wa kupeleka nyumbani." Ambalo, ninawapenda kuliko nyama yoyote iliyopo ya kula. Nami nikasema, "Laiti ningalipata tu watatu zaidi." Nikatembea mwituni mbele kidogo. Na, loo, hapakuwapo na yeyote. Wawindaji wazuri, kama Charlie na hao wengine, walipata mmoja. Nami nikasema, "Vema, mimi . . . "

116 Kitu Fulani kikasema, "Iambie. Wanene hao kuchakulo watatu nawe utawapata."

117 Nikasema, "Hilo limetendeka wakati mmoja." Kwa hiyo nikasimama kando ya mti mdogo, karibu mwisho wa alasiri, kando ya kigongo.

118 Ndipo huo Upako ukaja kwa nguvu sana hata ilikuwa vigumu kwangu kusimama juu ya ardhi, na kusema, "Nena! Usemayo, usione shaka, nawe unaweza kupata uliyosema."

Nikasema, "Nitapata kuchakulo watatu."

Yeye akasema, "Watatokea wapi?"

119 Nikasema, "Mmoja atatokea upande *ule*, mmoja kutoka kule, na mmoja nyuma *huku*." Kulifanya changamano. Mungu hajali jinsi linavyoonekana changamano. Yeye ni Mungu wa hali ya mambo.

120 Basi nilipokuwa nimesimama pale kwa yapata dakika chache. Sikuweza kusikia mlio wa risasi huko, hao wavulana wengine, popote pale. Ikawa niliangalia nyuma yangu, huko juu kabisa msituni, yapata yadi tisini, nilifikiri kitu fulani kilikuwa kwenye kisiki. Nikakiangalia. Baada ya kitambo kidogo kikaruka, na ilikuwa ni kuchakulo wa kijivu. Mbali sana, kote kupitia hilo bonde, na juu ya hicho kigongo. Alipokuja kando ya huo mti, nikampiga risasi. Na ilikuwa yapata yadi tisini, na ikamwua. Nikasema, "Huyo hapo mmoja. Afadhali nigeuke na kuangalia upande huu mwingine, kwa ajili ya hao

wengine, maana wanakuja." Mnaona? Mungu anayo njia ya kukuletea vitu, akikuhakikishia yale unayozungumzia.

121 Upako huo ulikuwa umenitoka wakati huo. Vema, nilingoja na kuangalia *huku* kwa yapata saa moja. Hakuna kitu kilichotokea. Nilikuwa ninaingiwa na baridi. Nikawazia, "Hakika, kama huyo ni Roho Mtakatifu ambaye ananiambia mambo hayo, itakuwa ni vivyo hivyo hasa. Kwa sababu, wakati huo Upako ulipokuwa juu yangu, nilinena neno hilo, na itabidi iwe hivyo."

122 Sasa sikilizeni hili kwa makini sana. Na hili litarekodiwa kwenye kanda. Litaenda ulimwenguni kote.

123 Mara kwa mara, kwenye mkono wangu wa kushoto, niliendelea kuangalia. Baada ya kitambo kidogo, nikaangalia juu. Juu ya mti mmoja, kuchakulo wa kijivu akatokea, akiuzunguka mfune. Nikasema, "Vivyo hivyo hasa. Hiyo ni kweli, Bwana." Nikashuka, nikasimama nipate kumpiga risasi, ndipo hapo akatokea kuchakulo mwingine. Nikasema, "Hao hapo wawili, vivyo hivyo hasa. Inafanya watatu wangu." Basi nikainuka, nikampiga risasi kuchakulo wa kwanza. Huyo mwingine akakimbia chini ya gogo. Ningeweza kumwona akipasua ko—kokwa ya hikori, ama kitu fulani, chini ya hilo gogo. Hilo gogo lilikuwa yapata juu *hivi*, mwishoni, limeinuliwa kama futi moja. Ningeweza kumwona huyo kuchakulo. Nikamwua yule wa kwanza.

124 Nikasema, "Sasa nitampata huyo mwingine." Nikalenga, nikaweka hiyo mistari iliyopitana papo hapo juu ya sikio lake, sio umbali wa zaidi ya yadi arobaini, hamsini, nikarusha risasi na kugonga lile gogo. Wala huyo kuchakulo hata hakusisimkwa. Nikaingiza risasi nyingine ndani. Naye akageuka, akaenda chini ya hilo gogo, akaenda upande huo mwingine. Vema, nikalenga na kupiga shabaha kadri nilivyoweza. Nami nilikuwa nimekosea risasi tano tu mwaka mzima. Kwa hiyo nikalenga, kupiga risasi kamilifu kabisa, ndipo nikagusa kifyatuo tena, nami nikapiga risasi yapata nchi nne juu yake.

125 Nikasema, "Hapana shaka niligonga darubini yangu ikaenda kombo." Ndipo basi nikaangalia tena. Huyo kuchakulo akapanda juu mbio akaenda upande wa msituni, kwa upana kutoka kwangu. "Vema," nikasema, "niliigonga darubini yangu ikaenda kombo. Nitampiga risasi kwa upana basi, kwenye kijishimo cha kifua." Basi nikaiinua na kuweka mistari ya kulengea. Nikawazia, "Labda nimeingiwa na baridi, na ninatetemeka." Nikawazia, "Sikuwa baridi na kutetemeka wakati nilipompiga risasi yule mwingine."

126 Kwa hiyo basi, vivyo hivyo tu, yapata muda wa dakika moja ama mbili. Nikashika kichaka, na kukiweka mkononi mwangu, na kuishikilia bunduki kwa nguvu sana, na kukilenga kijishimo, kijishimo cha kifua cha huyo kuchakulo, na kuivuta bunduki.

Ndipo nikapiga risasi futi moja chini yake. Ndipo nikavuta niingize risasi nyingine, nayo bunduki ilikuwa tupu. Wakati nikitia risasi, nilisema, "Nitampata endapo atasimama pale." Ndipo niliponinii . . .

127 Huyo kuchakulo akapanda kupitia mwituni. Nikasimama pale. Nikawazia, "Kitu gani? Hizo hapo risasi tatu, moja kwa moja, zimekosea. Nami nimekosea tu mara tano kutoka kwa mia moja na kumi na nne." Nikasema, "Ingewezekanaje, kwamba bunduki yangu ingekuwa kombo?"

128 Ndipo papo hapo likanijia. "Huwezi kumpiga kuchakulo huyo risasi hivyo. Alipaswa atoke upande *ule*." Neno la Mungu ni kamilifu. Nisingeweza kumpiga risasi kutoka kusini. Alikuwa atoke kaskazini.

129 "Loo," nikasema, "Nitageuka tu *hivi*, basi, na kuangalia kaskazini hata atakapotokea." Nikaweka risasi zingine kwenye bunduki, na kuangalia. Maskini . . . Nikasema, "Kama akija, itabidi awe karibu sana." Sipendi kumpiga risasi aliye karibu. Haifurahishi. Si vizuri kufanya hivyo. Kwa hiyo mmoja alikuwa . . . kile kichaka pale, nikasema, "Vema, itabidi nimpate huyu kutoka kaskazini, maana nilisema hivyo." Kwa hiyo nikasimama *hivi*, nikiangalia.

130 Nami ni—nikasema, "Nadhani . . . nimechelewa." Nikasema, "Saa kumi kasorobo, sasa ni saa kumi. Itanibidi kuondoka, kwa sababu, nikiwa na hao wawili, kwa sababu wale wavulana wananingojea." Na kwa hiyo nikangojea kidogo. Saa kumi ikafika, saa kumi na dakika tatu.

131 Nikasema, "Vema, nitaenda nikawachukue kuchakulo wangu." Nikapanda nikawachukua hao kuchakulo, nikarudi, giza sana ilikuwa ni vigumu kuona kwenye hilo bonde. Nikaanza kushuka bondeni. Ndipo nilipokuwa nikishuka bondeni, kulikuwa na giza, nami nilikuwa nimepita mahali nilipokuwa nimesimama.

132 Kitu Fulani kikaniambia, "Hivi hupandi kwenda kule juu kumchukua yule kuchakulo?"

133 Nikasema, "Ningewezaje kumwona sasa?" Nikiwa na maskini jicho dogo la darubini, darubini ndogo sana, nzuri, ya shabaha; karibu hakuna nuru ya kutosha kuona, futi chache mbele yangu. Nikasema, "Ningewezaje kumwona?"

134 Kasema, "Lakini ulisema ya kwamba kungekuwako na mwingine." Loo, laiti ningeweza kufanya hilo, kwa namna fulani ningepata, kuona hilo, naam, hilo, kile hilo linamaanisha hasa, rafiki. Mnaona? Chini ya Upako huo, sio mimi niliyesema hilo. Ilikuwa ni Mungu aliyelisema. Nami nikatembea hatua chache. Kasema, "Geuka urudi nyuma kuelekea kaskazini. Kuchakulo wako yuko huko."

Nikaenda, nikageuka. Nikasema, "Bwana Mungu, sitatilia shaka, hata kidogo."

135 Nikaanza kurudi nyuma kuelekea kaskazini. Kuna wale wanaoketi hapa wanaojua jambo hili. Nikaanza kwenda upande wa kaskazini. Na huko juu kabisa kwenye kigongo, umbali wa futi hamsini ama sitini, kuchakulo akakimbia juu mtini, nuru tu ya kutosha hata ningeweza kumwona. Nikatafuta kwa darubini yangu, kote juu na chini ya huo mti. Hakuna kuchakulo, ningeweza kumwona. Baada ya kitambo kidogo nilifikiri niliona kifundo kwenye mti, huko juu kabisa, giza sana. Nikasema, "Vema, nitajaribu hicho, kwa vyovyote vile." Nami nikapiga risasi. Basi nilipoipiga, kuchakulo akauzunguka huo mti mbio kisha akakimbia chini. Nikamsikia akianguka chini. Nikafikiri aliruka.

136 Wakati ule ule hilo lilipotendeka, yapata futi ishirini kutoka kwake, mmoja akapanda upesi mwaloni mweupe. Nilisema alishuka chini ya mmoja na kupanda juu ya mwingine. "Sasa, hakika, Bwana, Wewe hutaniacha nimkose, nikiisha kusema chini ya ule Upako ya kwamba huyu angekuwa ndiye. Nawe unaithibitisha huduma yangu. Hii itakuwa ni mara sita ambapo Wewe umenithibitishia." Namba ya mwanadamu, mara *sita*. Nikasema, "Hutaniacha nimkose." Nikaangalia, kote juu na chini ya huo mti. Na huko juu kabisa mle ndani, nilidhani niliona baadhi ya majani. Niliona kitu fulani kikijongea ndani yake. Nikainuka na kupiga risasi. Naye huyo kuchakulo akaanguka chini, amekufa fofofo. Mimi huyo, nikapanda kilima nikishangilia na kufurahi.

137 Nikaenda kwenye ule mti wa kwanza, mkono wangu wa kushoto, na *hapo* alilala huyo kuchakulo. "Vema," nikasema, "Ninajua nimempata huyo, bali sikuwa na hakika na huyu." Nikasema, "Basi, Bwana, umenipa mmoja wa ziada."

138 Ninaenda kule kumtafuta kuchakulo huyo mwingine, hakuwapo. Nami nikaangalia, na kuangalia, nikatafuta chini ya majani na kuinua vipande vya takataka, na kupasua gogo la kale. Wala hapakuwapo ila gogo moja lililokuwa ndani ya yadi thelathini, nami nikalipasua lote vipande-vipande. Nikaangalia chini pande zote, na kushika majani kwa mikono yangu, nikayapapasa. Hapakuwapo na kuchakulo pale, popote.

139 Huko juu, kulikuwako na kisiki kikubwa kilichojificha juu ya kilima. Nikapanda, maskini kisiki hicho. Palikuwapo na shimo dogo. Nikaingiza mkono mle ndani, nami nikadhani nilimgusa kuchakulo wangu, akiinuka juu chini. Nilipokuwa . . . nikasema, "Vema, siwezi kumfikia. Kwa hiyo, asubuhi, nitawarudisha hao wavulana na kumchukua. Sina budi kwenda kuwaambia." Ndipo nikashuka kwa Ndugu Charlie. Nikalishindilia hilo shimo, nikashuka kwa Ndugu Charlie na hao wengine, na kuwaambia.

140 Tukaenda nyumbani mwao usiku huo, kwa ajili ya chakula cha jioni. Tulikuwa tukishangilia katika Uwepo wa Bwana. Ndipo wakati, kabla ya kwenda kulala, Ndugu Charlie pale akamwomba Ndugu Tony Zabel, huko nyuma, kuongoza kwa maombi.

141 Sasa, sisemi hili kumgombanisha ama kumwudhi Ndugu Tony. Yeye ni mmoja wa Wakristo waungwana wazuri sana niwajuao. Lakini, kuwaonyesha tu jinsi Bwana anavyofanya kazi. Tony, katika maombi yake usiku huo, alisema, "Bwana Mungu, na ijulikane kwetu ya kwamba ndugu yetu anatwambia ukweli, ya kwamba kesho atampata huyo kuchakulo ndani ya kile kisiki." Hiyo ilikuwa . . .

142 Kamwe sikusema nitampata kuchakulo kwenye kile kisiki, chini ya huo Upako. Nilisema, "Nilimpiga risasi kuchakulo." Hakika, nisingempata huyo kuchakulo, kwa sababu, kama ningalimpata, hiyo ingewafanya wengi kuliko niliokuwa nimesema. Vile vile hasa nilivyokuwa nimesema, chini ya Upako huo, hao ndio Mungu aliowatoa. Kwa hiyo, sikusema lolote kuhusu hilo.

143 Mnaona, hivyo ndivyo, mara nyingi, watu wanasema, "Ndugu Branham alisema *hivi na vile*." Wakati Ndugu Branham anaposema lolote, hilo halina uhusiano wowote nalo. Lakini Mungu anapolisema, hilo ni kweli Milele.

144 Lakini Ndugu Tony hakulipata. Yeye alisema, "Endapo kuchakulo huyo yuko, basi tutajua ya kwamba ndugu yetu ametwambia ukweli." Ndugu Wood, Ndugu Charlie, wote hao, wakalichukua. Hatukusema chochote. Nililala pamoja na Ndugu Tony usiku huo.

145 Kesho yake asubuhi, mezani, tulikuwa tukizungumza, kuhusu, "Loo, ilikuwa ni siku mbaya sana."

146 Naye Ndugu Tony akasema, "Vema, kuna jambo moja, Ndugu Branham labda atatoa wake kutoka kwenye kisiki, asubuhi ya leo, kutoka kwenye huo mti."

147 Nikasema, "Ndugu Tony, kamwe sikusema huyo kuchakulo alikuwa mle ndani. Nilisema ningeweza kumgusa, wakati alipoinuka, angeshuka."

148 Akasema, "Atakuwako. Atakuwa mumo humo katika hicho kisiki." Tukapanda kule. Ndipo nilipoliacha gari, nilianza kurudi tena na kusema, "Kuna kasoro fulani. Afadhali nimwambie Tony sasa. Kwa sababu, ikiwa huyo kuchakulo hayuko kwenye shimo hilo, katika kisiki hicho, nirudi bila kuchakulo kabisa, basi kulingana na vile alivyoomba jana usiku, angali ataamini nilisema uongo." Nikasema, "Mungu, Wewe unajua, nikiwa na Biblia yangu, ya kwamba nimesema ukweli kabisa." Naye Mungu anajua hiyo ni kweli, nilisema tu ukweli.

149 Nami nikaendelea mbele. Kitu fulani kilinisukuma tu mbele. Nami nikaenda kupitia msituni, nikiwinda. Nikaendelea kuwazia, "Vipi kama kuchakulo huyo hayupo?" Alinipa kisu chake cha kuwinda, nikalipasue hilo shimo, nipate kuingiza mkono ndani na kumtoa.

150 Ndipo kitu Fulani kikaniambia, "Iwapo hayuko mle, ama kama yuko mle, inaleta tofauti gani?"

151 Nikasema, "Yeye ataninii . . . Hataniamini. Aliomba na kusema, kwamba, 'Kama tukimpata huyo kuchakulo, mtajua ya kwamba ndugu yetu alitwambia ukweli.'"

152 Ndipo ule Upako mkuu ukaja, kasema, "Sema tu huyo kuchakulo atakuwapo, nawe utampata."

153 Nikawazia, "Hakika, Bwana, hakika hii itakuwa ni mara saba, moja kwa moja, wakati Upako huu ukiwa juu yangu." Nikasema, "Huyo ni Wewe?"

Akasema, "Sema utakalo."

Nikasema, "Nitampata kuchakulo huyo." Huo Upako ukaniacha.

154 Nikawinda mpaka saa tatu u nusu, jinsi tulivyopaswa kufanya. Nilipokuwa nikishuka, na kwenda kuwachukua mbwa kadhaa basi, walidhani walikuwa. Ndipo nikapanda kile kilima saa tatu u nusu, nikaangalia lile shimo, nikapapasa pande zote, nikalikata. Hapakuwapo na kuchakulo pale, hata kidogo, shimoni. Nikapapasa kote. Sasa, kile nilichokuwa nikiokota kilikuwa ni mizizi ya nyasi ndogo nyororo, au mizizi ya miti niliyokuwa nikiokota, na kuihisi ikianguka kutoka kwenye hicho kijiti, nilipokiingiza hicho kijiti ndani, na kukivuta juu namna *hiyo*. Nilidhani nilikuwa ninamwokota yule kuchakulo. Naye alikuwa akitelezea kijitini, bali ni mizizi midogo na kadhalika. Hakuna kuchakulo mle. Nikawazia, "Sasa nitafanyaje?"

155 Nikasema, "Hii hapa, saa tatu u nusu. Sina budi kurudi." Nikachukua bunduki yangu nikaanza kushuka chini ya kilima.

156 Ndipo kitu Fulani kikasema, "Hivi hukusema utampata yule kuchakulo?"

Nikasema, "Nitampata wapi?"

157 Mungu akiwa ndiye hakimu wangu mkuu, pamoja na Neno Lake hapa. Nami ni mtu mwenye umri wa miaka hamsini, mhubiri wa Injili, nikisimama kwenye mimbara hii. Kitu Fulani kikasema, "Angalia chini ya kile kipande kidogo cha ganda."

158 Nikasema, "Bwana, kamwe nisingekutilia shaka kwa chochote." Nikaenda pale na kuinua hilo ganda, wala hapakuwapo na kuchakulo pale. Nikawazia . . .

Kabla tu sijafanya hivyo, kitu fulani kikasema, "Vipi kama hayupo?"

159 Nikasema, “Loo, atakuwapo.” Nikaliinua juu wala hapakuwapo na kuchakulo pale. Nikaangalia chini, kwa mshangao. Nikaona kipande kidogo cha kijivu kikitokeza chini ya jani. Nikakivuta, na huyo hapo yule kuchakulo. Ikilifanya kweli kabisa, kile alichokuwa amesema nifanye.

160 Mimi huyo nikashuka kilimani na kuwaambia habari zake, tukashangilia. Ndipo nilipofika kwenye gari, Charlie akisimama pale pale, Banks. Walikuwa wakizungumza. “Hilo si lilikuwa ni ajabu kwamba Tony angesema kitu kama hicho katika maombi yake, kadiri anavyompenda Ndugu Branham? Basi kwa nini angelitilia shaka neno lake na kuomba namna hiyo?” Mnaona, ilibidi tu aliseme hivyo, kwa kuwa Mungu alijua ya kwamba ningesimama mimbarani asubuhi ya leo na kudai kitu kile kile. Inakupasa kuangalia yale mwanadamu asemayo, kisha yale Mungu asemayo. Mungu asemayo ni kweli.

161 Kisha nikawazia, “Vema, Mungu asifiwe!” Nikashuka chini. Tulikuwa na wakati mzuri sana. Nikaja nyumbani.

162 Ndugu George Wright, kwa miaka mingi, ametengeneza divai ya ushirika. Halafu ninafunga. Ametengeneza divai ya ushirika kwa ajili ya kanisa. Ndugu Roy Roberson huko nyuma, akanipigia simu na kusema, “Ndugu Branham, hebu tushuke tukachukue divai ya ushirika kwa Ndugu Wright,” ambaye ameketi hapa, yeye pamoja na familia yake.

Sasa sikilizeni hili kwa makini, tunapofunga. Ee Mungu!

163 Tukafika kwa Ndugu Wright, mapema asubuhi, na, kama kawaida, ukaribisho mkubwa ukafanywa. Nasi tukazungumza juu ya hiyo divai. Ndipo maskini Edith, maskini yule msichana kiwete ameketi pale, ambaye nampenda, kama tufanyavyo hapa maskanini; sio mimi tu, bali maskani hii, kana kwamba alikuwa ni dada yetu wenyewe. Familia ya Wright imekuwa ndiyo familia ya siku nyingi sana, moja yazo, pamoja na akina Slaughters hapa. Roy Slaughter na hao wengine, na akina Wrights, ama Bibi Spencer, hao walikuwa miongoni mwa wale wa siku nyingi sana humu maskanini. Nafikiri akina Wrights wamekuwa wakija hapa kwa muda wa miaka ishirini na mitano ama ishirini na sita.

164 Niliomba na kuomba, kwa ajili ya msichana huyo mdogo. Nimeomba, kumwona Mungu akimponya. Nami nimeona mateso, hata makubwa kuliko yake, yakiponywa. Nami nimefunga, na nimeomba, na nimetamani, na nimemtafuta Bwana, kwa machozi, kwa ajili ya uponyaji wa msichana huyo mdogo. Maskini jamaa huyo mdogo aliteseka wakati alipokuwa mtoto mchanga, labda kupooza kwa watoto, ambako kumeikunyatisha maskini mikono yake na miguu. Aliteseka kwa miaka mingi. Ndipo tulipoomba kwa mara ya kwanza, kwa ajili yake, aliacha kuteseka. Huo ni mwaka. . .miaka ishirini na sita iliyopita. Anapoumwa na tumbo, ama kuumwa na jino,

mara tu tunapoanza kumwombea, ninajua Bwana atayaondoa. Lakini mateso hayo . . .

165 Nami nimemwona ameketi humu ndani jengoni, wakati viwete wengine wangesimama na kuondoka wakitembea, na mateso na kadhalika. Na kushangaa, "Ni kwa nini maskini msichana huyo asitembee? Bwana, mwonekanie. Jalia Malaika wa Nuru amtie uvuli huyo mtoto, nipate kusema, 'BWANA ASEMA HIVI.'" Kama ingalikuwa ni juu yangu, ningelinena. Lakini sio juu yangu. Ni juu Yake. Nami nikaangalia hilo.

166 Nasi tulikuwa tumerudi, alitaka sungura. Mimi na Ndugu Wood tukaenda na kuwaua sungura wawili, tukamletea. Alikuwa ametayarisha chakula cha jioni, Bibi Wright na hao wengine.

Basi kwenye wakati huo . . .

167 Dada Hattie Mosier, ndio kwanza ampoteze mumewe. Niliwaoza hao mume na mke, miaka kadhaa iliyopita. Wana watoto wawili wazuri. Naye Ndugu Watt aliuawa. Mvulana wake mwenyewe alimkuta chini ya trekta yake, amepondwa-pondwa hata akafa. Ndipo maskini mvulana huyo akarukwa na akili, na jambo fulani likampata. Mimi na Ndugu Wood tulienda kule usiku mmoja, na tukakaa usiku kucha, ambako mama yake na mjomba wake walikuwa wakikaa pamoja naye. Ndipo Mungu akampa afya, naye ameketi hapa asubuhi ya leo. Mama yake alimjali. Umri huo wa utineja, ndio kwanza aanze kuambatana na ulimwengu, umri wa miaka kumi na mitano, ama kitu kama hicho. Ndugu yake mdogo anakaribia umri wa miaka kumi na miwili, kumi na mitatu.

168 Dada Hattie Wright, nyote mnajua. Tunamwita Wright. Jina lake ni Mosier. Lakini amekuwa ni mtu mwaminifu. Maskini mke nyumbani, anaishi katika vyumba viwili, huko nyuma kabisa vilimani. Huko nje akiwa na sepetu na jembe, akijaribu kuondoa magugu kwenye shamba dogo la mahindi, kuiweka maskini familia yake ndogo pamoja. Amefanya kazi kwa uaminifu.

169 Nilipokuwa nimeketi mezani, nikila chakula cha jioni, nilikuwa nikielezea kwamba imani ni kitu gani. Nikasema, "Nayo imani ni namna hii. Kama ningeliona ono la Ndugu Shelby ameketi *hivi na hivi*, na kila mmoja jinsi walivyokuwa." Naye Dada Hattie alikuwa ameketi huko nyuma kabisa, kuelekea chumba kingine. Hakuwa na mengi ya kusema. Kamwe hawi nayo.

170 Ndipo wakati tulipokuwa tukizungumza, ningesema, "Kama Bwana alinionyesha ono ya kwamba jambo fulani lilikuwa litukie, basi ningeninii, ningelisema. Hilo ndilo linaloinua imani yangu." Nikasema, "Wakati Bwana anaponionyesha kile kitakachotukia, basi nina imani. Itakuwa hivyo."

171 Wakati aliponionyesha, nilisema, "Ningekuja papa hapa, kama maskini msichana huyo anayeteseka, aliyeketi pale, naye Bwana alinionyesha ya kwamba atapona. Ningekuja papa hapa na kusimama kwenye njia, nione kama kila kitu kilikuwa jinsi hasa alivyosema. Kisha niseme, 'BWANA ASEMA HIVI. Edith, simama utembee.'" Nikasema, "Mngeiona maskini miguu hiyo midogo ikikunjuka, maskini hiyo mikono ikikunjuka. Naye angesimama kutoka hapo na kutembea, kwa utukufu wa Mungu," nikasema, "kama lingekuja namna hiyo." Nilikuwa nikiwaambia kuhusu tukio hili. Ndipo nikasema, "Hivi mnajua. . .Ninataka kuwaulizeni jambo fulani." Ndugu Banks Wood alikuwa ameketi karibu nami, mezani. Naye aliyefuata, kuketi, basi, Dada Hattie alikuwa ameketi huko nyuma kabisa. Nao hao wavulana walikuwa wameketi hapa, na Bibi Wright, na Bw. Wright. Naye Shelby ameketi nyuma mkono wangu wa kushoto.

172 Sasa sikilizeni. Msilikose hili; niwaonyeshe ukuu wa Mungu.

173 Ndipo tulipokuwa tukizungumza, nilisema, "Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Ni kitu gani kilichowaweka hao kuchakulo pale? Hakuna kuchakulo msituni. Nilikuwa nimewinda na kuwinda. Na mimi—mimi siye mwindaji mzuri kuliko wote, bali nimewinda tangu nilipokuwa mvulana mdogo. Nami nilikuwa nimewinda sana, na—na walikuwa mahali pasipowazika kabisa, na kwa njia isiyowazika sana ningaliweza kuwaita." Nikasema, "Ni kitu gani kilichowaweka mle?"

174 Nikasema, "Sijui kama ni kwamba, kwamba huduma yangu iko karibu kubadilika, ya kwamba Mungu wa Ibrahimu anaithibitisha ahadi Yake, kama alivyofanya kwa Ibrahimu hapo alipokuwa juu ya ule mlima naye alihitaji sadaka, badala ya mwanawe. Yehova-yire alifanya mwujiza, na kuweka kondoo dume, maili mia moja huko nyuma. Alikuwa safari ya siku tatu. Na mtu yeyote wa kawaida anaweza kutembea maili ishirini na tano kwa siku. Ndipo akainua macho yake na kuuona ule mlima kwa mbali. Ndipo basi akaenda kwenye huo mlima, na akapanda juu ya mlima. Wakati, kondoo dume huko nyuma, kondoo, wanyama mwitu wangelimwua. Halafu, tena, huko juu ya mlima mahali pasipo na maji. Huyo kondoo dume alifikaje huko juu? Ilikuwaje? Mungu alihitaji sadaka, kumthibitishia Ibrahimu ya kwamba Yeye alikuwa ni Yehova-yire. Mungu yeye yule wa uumbaji alinena kondoo dume akawa. Sasa, halikuwa ni ono. Yeye alimwua huyo kondoo dume, na damu ikamtoka mnyama huyo. Halikuwa ni ono. Alikuwa ni kondoo dume."

175 Nikasema, "Mungu yuyo huyo," haleluya, "huyo Yehova-yire, Yeye ni Yehova-yire siku hizi kadiri tu alivyokuwa kwenye ule mlima pamoja na Ibrahimu." "Yeye angali anaweza kumtoa mnyama, kwa ajili ya utukufu Wake. Kuchakulo hawa hawakuwa ni ono. Niliwapiga risasi. Damu iliwatoka. Nikawachinja na kuwala. Hawakuwa ni maono. Walikuwa

ni kuchakulo." Nikasema, "Yehova-yire yuyo huyo, akijaribu kuniletea ahadi Yake, katika uvivu wangu na uzito wangu wa akili, Yeye angeweza kunena haja yangu ikawa, vile vile kama alivyoweza kuinena haja ya Ibrahimu ikawa."

176 Mara niliposema hivyo, basi. . .Dada Hattie, ameketi pale akilia sasa, hakuwa amesema neno. Ndipo akasema, "Hiyo ni kweli tupu."

177 Alisema jambo lifaalo. Alisema kama tu vile Banks alivyosema huko chini. Niliisikia sauti yake, wakati ikipitia masikioni mwangu, kama vile huko msituni.

178 Bibi Wright, aliyeketi pale nyuma na msichana wake mdogo, alikuwa akijaribu kufasiri yale Edith aliyosema. Nisingeweza kumsikia Bibi Wright.

179 Ndipo Upako ule maalum ukashuka juu yangu, kasema, "Mwambie Hattie ya kwamba amepata neema machoni pa Mungu." Ni nani angaliweza kuwazia? Kasema, "Mwambie aombe lolote atakalo. Kisha wewe ulinene, kwa karama hii, liwepo. Lolote atakaloomba, linene liwepo."

180 Nikamwangalia Dada Hattie. Mara ya kwanza lilipotendewa mwanadamu. Nikasema, "Dada Hattie, omba utakalo. Mungu atakupa."

181 Mnawazia nini juu ya hilo? Linawaingia? Mara saba alikuwa amelithibitisha, kwa mnyama. Saba ni nambari kamili ya Mungu. Hapa ndiyo mara ya kwanza juu ya mwanadamu. Na, Yeye, Yeye alichagua nini, kabaila mashuhuri, mhudumu mkuu mwenye sifa? Maskini mjane ambaye angeandika jina lake kwa shida. Mungu anajua yale anayofanya.

Kasema, "Omba utakalo."

Hattie akaniambia, "Ndugu Branham, unamaanisha nini?"

182 Nikasema, "Omba lolote unachotamani moyoni mwako, nacho kitatolewa papa hapa, upate kujua ya kwamba Bwana Mungu wa Mbinguni hujibu, nayo Maandiko Yake ni ya kweli."

183 Mara yangu ya kwanza nikiwa na ile karama mpya; Upako wangu wa kwanza. Nilimsikia kwa shida. Naye akaangalia pande zote. Tulikuwa tukizungumza juu ya maskini dada yake mdogo, kiwete. Nikasema, "Loo, hapana shaka," moyoni mwangu, "katika dakika chache maskini Edith atakuwa akiruka-ruka kwa utukufu wa Mungu."

184 Hattie akaangalia kote, pande zote. Naye akasema, "Ndugu Bill, shauku yangu kuu kuliko zote ni wokovu wa wavulana wangu wawili." Ni ninii. . .Mbona, kusingeweza kuwa na jambo kuu zaidi. Angaliweza kuomba dola elfu kumi, angezipata. Vipi kama ingalikuwa ni milionea fulani angeomba milioni nyingine moja? Mungu alijua kile alichokuwa anaenda kuomba.

185 Dada Hattie, angalau, mashahidi saba ama wanane wamesimama pale. Ninyi watu wote mliokuwapo wakati hilo lilipotukia, inua mkono wako. Kila mtu jengoni, aliyekuwapo, hilo lilipotukia; moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. Saba wa hao. Wanane wao. Wanane wao walikuwako wakati hilo lilipotukia.

186 Nikasema, "Omba lolote utakalo. Maana, Mungu amenipa mimi, nipate kukupa wewe, chochote utakacho."

187 Alisema wavulana wake walikuwa wakianza kwenda kombo kwa hamaki ya utineja. Ndipo akasema, "Wokovu wa wavulana wangu wawili."

188 Nikasema, "Kwa mapenzi ya Mungu, kwa Nguvu za Mungu, ninakupa, katika Jina la Yesu Kristo, shauku yako." Ndipo wavulana wake wawili wakatetemeka chini ya Nguvu za Mungu. Nalo jengo hilo lote likatetemeka. Banks akaangukia sahani yake. Shelby akashika ghafla. Naye Hattie akapiga mayowe hata ungeweza kumsikia kwa majengo mawili. Nao hao wavulana wawili, huku machozi yakitiririka mashavuni mwao, wakapokea kile hasa walichoomba, papo hapo. Loo!

189 Mara ya kwanza ilipotumiwa kwa mwanadamu. "Ombeni mtakalo, nanyi mtapewa." Wavulana wake, wameketi pale pamoja naye, asubuhi ya leo.

190 Yeye angaliomba kitu gani? Vipi kama angaliomba uponyaji wa maskini dada yake? Vipi kama angaliomba hilo? Msichana huyo mdogo angaliponywa, lakini wavulana wake wawili wapotee. Vipi kama . . .

191 Mjane huyo maskini, ambaye ndio kwanza aniambie ya kwamba alijaribu kulipatia kanisa hili dola hamsini kwenye ahadi, kusaidia kujenga kanisa jipya. Naye Ndugu Roberson asingeweza kuzichukua, akamruhusu tu kutoa ishirini zake. Nami nikajiambia, alipokuwa akizungumza, "Nitamrudishia hizo ishirini."

192 Lakini Mungu akaniambia, moyoni mwangu, sasa, sio kwa ono, moyoni mwangu, "Wakati Yesu alipokuwa amesimama, akimwangalia mjane akiweka senti tatu, ambako kulikuwako na maelfu ya dola mle, wewe ungalifanya nini?"

193 Nikasema, "Vema, kama ningalikuwa nimesimama pale, ningesema, 'Hatuzihitaji hizo, dada. Tunazo pesa nyingi.'" Lakini Yesu kamwe hakusema hilo. Alimwacha aendelee na kufanya hivyo, kwa sababu Yeye alijua kile kilichokuwa huko mbele safarini.

194 Kwa hiyo nisaidie, Mungu akiwa hakimu wangu mkuu, Mungu alijua kilichokuwa huko safarini kwa ajili yake. Ndipo nikaweka mkono wangu mfukoni mwangu, kutoa kitabu changu cha mfukoni, kumrudishia dola zake ishirini, na kusema, "Dada Hattie . . ."

Lakini Yeye akasema, "Usifanye hivyo."

195 Halafu dakika chache, wakati swali limeletwa juu ya Yehova-yire, yeye alisema, "Hiyo ni kweli tupu." Nayo yalitoka moyoni mwa mjane maskini, Mungu akijua angeomba kitu kikubwa kuliko vyote kinachoweza kufanywa. Mradi tu kunayo Mbingu, nyota zitakapokwisha, wakati mwezi haupo tena, hakuna dunia tena, hakuna bahari tena, hao wavulana wataishi katika Umilele pamoja na Yehova-yire Yeye yule aliyetoa hiyo ahadi isiyopatikana na mauti. Ahadi Zake haziwezi kushindwa.

196 Ninatarajia kuja kwa mkutano huu hapa chini katika San Jose. Loo, laiti ungalitokea! Sasa huo Upako unaposhuka, "Omba utakalo." Ninalo hakikisho kamilifu ya kwamba Huo unaposhuka, na lolote Mungu analoweka lipate kuombwa, itakuwa vivyo hivyo hasa. Halina budi kuwa, "Kwa kuwa ukiuambia mlima huu."

197 Mnaona, si wewe unayenena. Sio wewe. Ni Mungu. Ni wewe, ume—umejisalimisha sana kwa Mungu.

198 Sasa waangalieni manabii wa kale, wakati tukifunga. Hao manabii wa kale, walipokuona kule Kuja kwa Bwana Yesu, walikuwa katika Roho sana hata wakanena kana kwamba ilikuwa ni wao wenyewe. Mwangalieni Daudi katika Zaburi, Zaburi ya 22, akilia, "Mungu Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Sio Daudi; ilikuwa ni Kristo, miaka mia nane baadaye. "Mifupa yangu yote inanikazia macho. Wananirushia midomo yao. Wanatikisa kichwa chao." Kasema, "Aliwaokoa wengine, lakini Mwenyewe hawezi kujiokoa." Daudi, akinena kana kwamba ilikuwa ni yeye mwenyewe. Lakini ilikuwa ni Roho wa Mungu ndani yake; Kristo, akinena.

199 Loo, Mungu asifiwe, anaingia Kanisani Mwake, katika utimilifu wa Nguvu Zake, akitenda kazi miongoni mwa watu Wake, akizitandaza mbawa Zake kuu za rehema. Na asifiwe!

200 Sina wakati kwa ajili ya mahubiri yangu. Na tuviinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

201 Kunaye mmoja hapa, asubuhi ya leo, ama ni wangapi wao waliopo hapa, wanaojua ya kwamba hamko tayari kwenye wakati huu kukutana na Mungu? Mnaweza kuinua mikono yenu, na kusema, "Uniombee, Ndugu Branham." Hatuwezi kuwaleta madhabahuni, maana madhabahu zimejaa watu. Mungu akubariki, ndugu; wewe, dada; wewe, ndugu; wewe, na wewe huko nyuma, pande zote; wewe, msichana mdogo; wewe, ndugu yangu; huko nyuma kabisa upande wa nyuma, pande zote. Mungu anaiona mikono yenu.

202 Iwapo Yeye anaweza kumleta kondoo dume awepo wakati hakuna kondoo dume, kama anaweza kuwafanya wanyama wawepo, kama anahusika juu ya maskini mtini unaokulia kando ya kilima, ama maskini samaki mdogo aliyekufa, aliye majini, ni zaidi sana vipi Yeye anajua shauku yako! Na ninii yako. . .

Hakika, Yeye anajua. Anajua kwamba unamhitaji. “Ombeni, nanyi mtapokea. Mwombapo, aminini kwamba mtapokea mlichoomba.” Je, huyo aliyeuinua mkono wako alikuwa ni Roho Mtakatifu? Kama alikuwa ndiye, basi ule Upako uko juu *yako*. Basi omba, na umwamini Mungu, nawe utapata ulichosema.

203 Baba wa Mbinguni, wakati siku hii ikikua kufikia adhuhuri, nami nimekuwa hapa kwa kirefu asubuhi ya leo, juu ya hadithi hii ya neema Yako ya Kiungu, kulingana na Neno Lako. Imeandikwa katika Maandiko, ya kwamba Yesu Bwana wetu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya.” Nasi tunajua ya kwamba kazi hizo ni za kweli. Ungeweza kupambanua mawazo ya watu. Ulimwambia Petro kwamba alikuwa ni nani, jina lake lilikuwa nani, baba yake alikuwa nani. Ulimwambia Filipo wakati alipomleta Nathanaeli, ama ulimwambia Nathanaeli, hasa, ya kwamba ulimwona chini ya mti kabla yeye hajaja. Ulimwambia yule mwanamke, kisimani, alikuwa na waume wangapi. Loo, hakuna kitu kilichofichika Kwako. Ulijua mambo yote. Na hizo zilikuwa ni kazi Zako. Halafu, tunakuona ukiuambia ule mtini.

204 Ee Bwana, ninaamini saa yaja hivi karibuni, ambapo mikate na samaki watazidishwa. Kutakuja alama ya mnyama, hivi karibuni. Kutakuja muungano wa makanisa. Nao watatoa ishara, kanisa la muungano, ambapo, “Hakuna mtu anayeweza kununua wala kuuza.” Nalo Kanisa lako, haitawasumbua, kwa kuwa Roho Wako Mtakatifu atawaongoza na kuwalisha, kama ulivyowafanyia Israeli nyikani. Wewe ni Mungu. Usituache tulikose hilo, Bwana. Jalia tubaki, waaminifu. Na tuwe wakweli.

205 Sasa sijui ni lini tu hili litakapotukia tena, Bwana. Labda asubuhi hii, tena. Labda litatukia tena maskanini leo hii. Nikitumainia kwamba litatukia, Bwana. Nikitumainia ya kwamba utaweka imani katika mioyo ya watu, na kujua ya kwamba sijakosesha ama kusema jambo moja baya. Nililisema jinsi tu lilivyokuja, vizuri nijuavyo moyoni mwangu, Bwana, nikiyaangalia maneno yangu na kuyapima. Nikijua ya kwamba Wewe umenithibitishia hilo, kama vile nilivyosema, mara saba. Na kujua, mara baada ya hayo, juu ya mwanadamu wa kwanza kabisa niliyepata kumnenea, alipata shauku ya moyo wake, mara aliponena.

206 Sasa, Bwana, kuna mahitaji mengi asubuhi ya leo. Itakubidi kumtia mafuta mtumishi Wako, Bwana. Laiti ungaliutuma huo Upako! Jalia niupate, asubuhi ya leo. Kama mtu angehitaji, Wewe liseme tu kwangu, Bwana, watakaponena, ama wakati wowote, yeyote umtakaye. Basi jalia litimie.

207 Sasa, ninajua kile kilichosemwa basi, haitakuwa ni mimi, itakuwa ni Wewe, Bwana, ukinena. Ninajitolea Kwako, na kabla sijaondoka kutoka kwenye huduma hii, ile ya zamani, ya maono na kadhalika, kwenye madhabahu haya, ambapo

niliyaweka maisha yangu wakfu upya; kuanzia kuhubiri Injili, hadi kwa ishara na maajabu. Ninajiweka wakfu tena asubuhi ya leo, Kwako, Bwana, kwa ajili ya utumishi. Wakati wa kwanza hili limesimuliwa. Mara ya kwanza, Bwana, ambapo imedhihirishwa. Hawa hapa mashahidi wameketi.

208 Ee Bwana Mungu, kukiwapo na chochote unachoweza kutumia maskini ganda hili langu kwake, mimi ni Wako, Bwana. Nichukue, na unifinyange, na unitengeneze, na kufanya jambo fulani, Bwana, ambalo litakuheshimu na kukutukuza Wewe. Lisambaze miongoni mwa wahudumu wengine. Litume kwenye pembe nne za ulimwengu. Saa zinachelewa. Yesu yuaja.

209 Wabariki watu Wako, pamoja. Waokoe waliopotea. Kila mtu aliyeinua mikono yao hapa, asubuhi ya leo, waokoe, Bwana. Wape Roho Mtakatifu. Jalia maisha yao yawekwe wakfu Kwako.

210 Maskini kanisa hili dogo, Bwana, mchungaji, na kila mchungaji aliye hapa, kila mwinjilisti, mwalimu, kila mfuasi wa kanisa lingine lolote. Ee Mungu, kama kundi la watu, tunajitolea Kwako. Tuchukue na ututumie, Bwana. Sisi ni wako, na tunatarajia kuja Kwako siku moja, katika amani.

211 Sasa iwapo kuna mgonjwa yeyote ama anayeteseka, jalia waponywe, asubuhi ya leo. Jalia neema Yako na baraka za Milele zikae juu yao, tunapowaombea, kwa kuwawekea mikono yetu na kuomba. Jalia Roho Mtakatifu aje na kufanya kazi ambazo amekusudia zifanywe. Lijalie, Baba. Kupitia kwa Yesu Kristo, tunaomba baraka hii. Amina.

212 Nimewaambia ukweli mtupu. Kama tu vile Mungu alivyoufunua, na ameufanya, nimewaambia ukweli kwa uaminifu. Na sasa ninatafuta kwa bidii na kuyatamani maombi yenu. Ninatambua ya kwamba mtu wa umri wangu, umri wa miaka hamsini . . .

213 Hivi majuzi asubuhi, nilimwambia mke wangu, "Tayari mimi nimefikisha hamsini, mpenzi. Kama nikimfanyia Bwana lolote, inanibidi kuharakisha."

214 Akasema, "Bill, Mungu alimfunza Musa miaka themanini." Kisha kasema, "Yeye anaweza kukufunza kwa miaka mingine hamsini, ili apate huduma ya siku moja kutoka kwako. Yeye ana kusudi kwa ajili yako, kwa hiyo simama tu kimya." Nilifikiri hiyo ilikuwa ni hekima nyingi, "Simama kimya."

215 Mungu husogeza kila mkono kulingana tu na mpango Wake mkuu. Simama tu kimya. Usijaribu kupita . . . kujaribu kusukuma. Unamtangulia, basi. Ni bora zaidi kujaribu kufuata kuliko ilivyo kuongoza, maana Yeye ndiye kiongozi.

216 Sasa, kwa maskini kanisa langu hapa, kundi langu dogo ambalo limekuwa aminifu sana, na limeniombea, kote ulimwenguni. Ninaamini kuna mtikiso mwingine wa ulimwenguni kote unaokuja. Mambo haya niliyowaambia ni

ya kweli. Kwenye Siku ya Hukumu, nitakabiliana nanyi huko ng'ambo pamoja na hadithi ii hii, kweli tu kama ninavyosimama hapa.

217 Sasa, nina hakika nyote mngeweza kuona ni kitu gani. Ni kule kuja kwa Upako mkubwa zaidi, wenye kilindi wa Roho Mtakatifu. Jinsi ya kuingia ndani Yake, sijui mimi. Jambo pekee nijualo, inahitaji Mungu kukuweka ndani Yake. Kwa hiyo, ishi kwa utamu tu, na kwa unyenyekevu, na karibu na Mungu kadiri uwezavyo. Usimtilie shaka. Amini tu kwamba kila kitu kinafanya kazi kwa manufaa, kwa ajili yako, na kila kitu kitatenda kazi pande zote vizuri. Unaona?

218 Kumbukeni tu, ninyi ni kondoo. Yeye ni Hua. Naye hua humwongoza mwana-kondoo. Wakati. . .Naye mwana-kondoo na hua wana asili ile ile. Hua ndiye aliye mpole sana kuliko ndege wote wa mbinguni. Mwana-kondoo ndiye aliye mpole sana kuliko wanyama wote wa duniani. Kwa hiyo, unaona, roho zao zingeafikiana. Sasa, hua asingeweza kuja juu ya mbwa mwitu. Mnaona? Asingeweza kukaa hapo. Mbwa mwitu ni mwuaji. Mwana-kondoo ni mpole.

219 Kwa hiyo, unaona, ni Mwana-Kondoo na Hua, na mmoja akimwongoza mwingine. Nanyi mnaona mahali Hua alipomwongoza Mwana-Kondoo? Moja kwa moja hadi Kalvari, apate kusulubiwa. "Wala hakufungua kinywa Chake." Walipomtemea mate, Yeye kamwe hakuwatemea. Walipompiga, Yeye hakuwapiga. Aliendelea tu moja kwa moja, akijua kwamba Yeye alikuwa, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, Yeye alikuwa akifanya mapenzi ya Mungu.

220 Dada Hattie, sisi karibu ni wa rika moja. Ndugu George Wright pale, baba yake, na wavulana wake, mama, Shelby.

221 Ninataka kusema jambo hili. Nadhani mnashangaa ni kwa nini niliamka na kwenda nje ya nyumba upesi nilivyofanya. Kamwe sijaninii. . .Nimekuwa mahali ambapo makafiri elfu thelathini waliokoka kwa wakati mmoja, Afrika Kusini, wakamjia Kristo. Nilidhani huo ulikuwa ndio Upako mkuu sana niliowahi kuuhisi. Kamwe, kwa njia yoyote, haukulingana na ule kule chini kwa George Wright, hivi majuzi. Sijawahi kuhisi kitu chochote kama Hicho. Chumba chote kilionekana kuwa tu Nu—Nuru ya Utukufu wa Mungu.

222 Sasa, Dada Hattie ni mnyamavu sana na maskini mwanamke mtakatifu, kamwe hainui sauti yake kuhusu chochote. Lakini ungaliweza kumsikia akipiga mayowe, jengo moja la mji, hapo Roho Mtakatifu aliposhuka kwenye hilo jengo. Kila mtu, kila mtu pale, alimhisi. Ilikuwa ni nzuri sana. Huenda tukaishi muda mrefu, lakini, Dada Hattie, maadamu kuna kumbukumbu niani mwetu, tutakumbuka hilo, na Dada Wright.

223 Sasa, ili kwamba watu wajue ya kwamba nilisimulia hayo kweli kabisa, waweza kuinua mkono wako, Dada Hattie, ili

kwamba, kwamba, Dada Wright na ninyi nyote mliokuwa kule, waliokuwa tu kule, ili kwamba tu mnaweza kuona. Mnaona? Hao hapo.

224 Hapa, simama, Dada Hattie. Huyo hapo maskini yule mjane ambaye huo muujiza ulimfanyikia, mara ya kwanza. Ukiwapita watu wote ulimwenguni, kwa jambo hilo kutokea kwanza kwa mjane huyo mdogo maskini, mnyenyekevu, huko juu ubavuni mwa kilima, huko juu akijaribu kukuza zao la mahindi kutoka kwenye eneo la kamba wa maji baridi huko nje, kuwashughulikia watoto wake. Huyo ndiye Mungu alimheshimu, kwa mara ya kwanza tangu siku za . . . za Yesu Kristo, na kusema, "Omba utakalo."

225 Nikasema, "Ninampa changamoto mtu yeyote, katika Jina la Bwana. Wakati Roho huyo anaposhuka na kusema hivyo, sijali utaomba nini, utapewa."

226 Mnajua ni kwa nini watawala wenye mali hawakulipata, ama jamaa wakubwa kama hao? Ni kwa sababu Mungu alijua wangeomba vitu visivyo vizuri kwao.

227 Yeye huwapa watu ambao anajua wataomba jambo linalofaa. Na ni kitu gani zaidi mwanamke huyo . . . Ni kitu gani zaidi? Niambieni tu kitu chochote angaliweza kuomba kikubwa kuliko hicho. Mama yake na baba yake wameokoka. Dada yake mdogo ameokoka. Familia yote imeokoka, isipokuwa hao wavulana wawili, wakati huo. Hawakuwa wameokoka.

228 Hao ni watu maskini. Shelby aliniambia mapato yake ya sikuzote, kwa zao zuri, alipata dola mia sita kwa mwaka. Akifanya kazi mpaka huyo mvulana ana karibu umri wangu, na amedhoofika kabisa, kila kitu. Huku akifanya kazi, akiwashughulikia baba na mama yake, nao ni wakongwe, na kujaribu kumshughulikia dada yake mdogo, anayeteseka. Lakini yeye ameokoka. Ndugu Wright, hao wote, wameokoka.

229 Lakini hao wawili hawakuwa wameokoka. Ndipo Hattie akaomba wokovu wa watoto wake, maadamu kuna Umilele. Angaliweza kuomba dola elfu kumi, na kuzipata. Angaliweza kuomba chochote alichotaka. Lakini Mungu anajua kile utakachoomba, kabla Yeye kamwe hajauweka Upako. Hiyo ni kweli.

230 Dada Hattie, ni kweli, kwamba nilisema, "Omba lolote utakalo. Lolote moyo wako utakalo, liombe, Hattie"? Hiyo ni kweli, Dada Hattie? Mnaona? Mnaona? "Omba lolote utakalo, haijalishi ni kitu gani. Liombe. Mungu ameniambia, 'Nena tu kile yeye ameomba, naye atakipata.'" Nikasema, "Kiombe sasa, chochote tu utakacho." Naye akafanya hivyo.

231 Loo, ndugu, dada, unaitambua siku tunayoishi? Wakati wenye utukufu kuliko wote, wakati Mungu wa Mbinguni ataweka miongoni mwa wanadamu, ati, "Omba lolote utakalo, Naye atakupa." Huh! Ni—ni ya kilindi kupita kiasi kwa akili

yangu. Ninajua hilo. Lakini ninatumaini, moyoni mwangu, ninaweza kupokea mengi Yake kadiri niwezavyo. Hilo, ni ninii tu. . .Nimeliishia. Nimeneemeka juu Yake. Ninaelekea magharibi juu Yake. Ninaingia mikutanoni juu Yake. Ninaishi juu Yake. Neno la Mungu ni kweli.

232 Sasa, nijuavyo mimi, hilo ndilo jambo la mwisho litakalotukia. Sijui jambo lingine lolote, kile lingeweza kuwa, kuwapa tu wanadamu, "Omba lolote utakalo, haidhuru ni kitu gani. Liombe tu, nawe utapewa."

233 Nawe ungeweza kuiona hiyo hekima? Ni wangapi wanaoamini hilo, ya kwamba mwanamke huyo aliomba kitu kilicho kikuu sana kilichoweza kuombwa? Hebu tuwaone. Ungeweza kuwazia? Mwa—mwanamke aliye na dada anayeteseka, angeweza kuomba uponyaji wake. Mwanamke ambaye ni maskini, na mama na baba yake, maskini, na hao wote maskini, angeweza kuomba pesa na kuzipata. Angeweza kuomba aongezewe miaka maishani mwake, na kulipata. Ila aliomba kitu kikuu kuliko vyote kingaliweza kuombwa, wokovu wa familia yake isiyookoka, naye akaupata. Amina. Hilo ndilo jambo muhimu. Akaupata, kwa Mungu yeye yule aliyetoa hiyo ahadi. Yeye ni Mungu. Loo, jinsi ninavyompenda!

234 Sasa tunaenda. . .Kunaye mgonjwa yeyote hapa wa kuombewa? Inua mkono wako. Mwanamke mmoja alipiga simu siku chache zilizopita usiku. Kunao watatu, ninaamini, kutoka California ama kitu kama hicho, waliniambia. Waliosema, "Tumekuja mara mbili ama tatu, nanyi mkasambaza kadi za maombi, nazo namba zetu haziitwi." Nilimtolea ahadi, endapo angebaki huku, ya kwamba ningewaombea tu wagonjwa asubuhi ya leo.

235 Ni wangapi wamekuwa hapa ndani wakati tumekuwa na upambanuzi na kadhalika? Loo, nyinyi nyote, nadhani, kila mtu hapa. Mnaona? Tunajua ya kwamba hiyo ni kweli. Tunaenda mbele kupita hapo sasa. Loo, sifa iwe kwa Mungu! Tunaenda mbele kupita hapo sasa. Labda itatimia. . .Sijui yale Mungu atakayofanya asubuhi ya leo.

236 Lakini ninyi watu mlio wagonjwa na mnaoteseka, nitawaomba tu mje, wachache kwa wakati mmoja. Hebu hawa upande huu *hapa,* wapande juu, kusudi tuweze kuwaombea hawa wa upande huu kwanza. Labda ninaweza kulishika namna hiyo. Njoo moja kwa moja hapa juu, dada. Fanyeni tu mlolongo papa hapa juu. Maana hatuna. . .Hawana budi kuwatuma warudi chini kwenye marefu ya kanisa, kwa kusudi la wao kurudi mahali pale pale.

237 Ningeweza kujua jinsi maskini jamaa huyu alivyozungumza, asubuhi ya leo, yeye anaamini katika uponyaji wa Kiungu, najua, na anaamini katika Nguvu za Mungu. Kuna mhudumu mwingine hapa, asubuhi ya leo, ambaye ni m—mhudumu anayeamini ya

kwamba Mungu huwaponya wagonjwa? Kama yupo, na aje huku juu, kila mmoja. Nyote njoni hapa na kusimama pamoja nasi wakati tunapowaombea hawa, hawa wagonjwa na wanaoteseka. Yeyote wenu ndugu mnaoamini ya kwamba Mungu huwaponya wagonjwa, Mungu akubariki, bwana, njoo moja kwa moja mbele. Tunataka uje papa hapa pamoja nasi.

238 Sasa hatujui yale Roho Mtakatifu huenda akafanya. Huenda Roho Mtakatifu, kwenye wakati huu, akafanya kama tu Yeye alivyofanya huko chini kwa Dada Wright siku ile nyingine. Natumaini kwamba atafanya hivyo. Sijui. Mnaelewa? Ni wangapi wanaojua...? Vema, hakuna wengi wenu mliosalia hapa, wakati yale maono yalipoanza kwanza. Sijui ni wakati gani yatakapokuja, yale yatakayofanya. Kila kitu kiko katika mapenzi ya Mungu na hakina budi kudhibitiwa na Mungu. Ni wangapi wanaojua hilo? Mungu asingeweza kuwapa wanadamu mambo ya kudhibiti, wenyewe. Kama wangalifanya hivyo, basi, isingekuwa ni Mungu. Isingekuwa ni Mungu. Ingekuwa... Ninawatakeni muwazie hapa, enyi marafiki, katika mahali hapa padogo na panyenyekevu, lakini jinsi Bwana kabisa, Ndugu Mike, bila tashwishwi yoyote, ametubariki, na kufanya na kutenda sawasawa kabisa na yale aliyoahidi Yeye angefanya.

239 Ni wangapi waliopata kusikia juu ya ufahamu usiowezekana kwa hisi? Wengi wenu mmesikia. Si—si kitu ila mitholojia, mizimu. Lakini, mnajua, hawawezi...Mambo hayo hayadumu. Hayashikilii. Wasingeweza kupata kitu chochote. Wataketi chini pale na kuwa na...Wanasema, “Kuna roho fulani. Kuna roho fulani.” Nao watajaribu kupiga picha yake, ama kitu fulani. Hawawezi kufanya hivyo. Mnaona? Ni kwamba tu haipo. Ni ya akili, ya kufikirika. Mnaona?

Lakini anachofanya Mungu ni kikamilifu.

240 Musa alipotupa chini fimbo yake, yule mchawi alitupa fimbo yake, pia. Zote mbili ziligeuka zikawa nyoka. Hiyo ni kweli? Lakini ilikuwaje kwa fimbo ya Yane na Yambre? Fimbo ya Musa iliimeza. Basi wakati Musa alipoichukua fimbo yake, ilikuwa ingali ni fimbo. Lakini fimbo yao ilikuwa wapi? Ndani ya fimbo ya Musa. Mnaona? Usingeweza kuiona. Mungu anapofanya lolote, Yeye hulifanya halisi.

241 Sasa wao wananiambia, “Roho Mtakatifu, wajua,” wanasema, “hao ni watu waliosisimkwa tu. Ni la kiakili. Hayo maono na kadhalika, hayo ni kuwasiliana tu kwa mawazo.”

242 Vema, wakati George J. Lacy alipochunguza picha ile kule, wakati huyo Malaika wa Bwana, wengi wenu mnaosimama hapa mlimwona huko mtoni, na mara nyingi. Yeye alisema, “Ndugu Branham, jicho la kimitambo la kamera hii haipigi picha saikolojia.” Kasema, “Nuru ilikuwako. Hiyo hapo.” Ni ya milele. Ni ya kweli. Kwa hiyo, mnaona, ni Malaika yule yule wa Mungu. Sasa hebu mwangalieni. Asili Yake inamthibitisha.

243 Wakati alipokuwa hapa duniani, Aliishi ndani ya Bwana Yesu Kristo, Ambaye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa. Na sasa Yesu alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo, ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Nayo mambo mfanyayo ninyi, niyafanyayo, ninyi nanyi mtayafanya.”

244 Sasa mwangalieni, anapokuja. Mwanadamu anaweza kusema lolote, bali Mungu anapoliunga mkono, hilo linalifanya kweli. Sasa angalieni asili ya huyo Malaika. Anapomfanya mtu kujitolea sana Kwake, Yeye hufanya jambo lile lile ambalo Yesu alifanya wakati alipokuwa hapa duniani. Kwa sababu, sisi ni wana na binti za Mungu, ikiwa tumezaliwa kwa Roho Wake. Mnaona? Wala sio kitu cha kubuni. Ana ushahidi wa kulithibitisha. Inaonyesha kwamba ni kweli. Kwa hiyo wokovu wetu ni mkamilifu kabisa.

245 Mungu wa Mbinguni, Yule aliyewafanya manabii wote kuzungumza juu ya Kuja kwa Bwana Yesu. Naye Yesu, alipokuja, Yeye alitimiza kila unabii. Mwingi wa huo ulitimizwa pale msalabani, “alijeruhiwa kwa makosa yetu,” na yale Daudi aliyosema, “Mungu wangu, Wewe umeniacha?” Lakini Mungu anapomtuma nabii, nabii hunena, Mungu anayafanya hayo kweli, iwapo ni Mungu. Hapo ndipo Yeye aliposema, kuwajua. “Kama walinena, na yale waliyosema yatimie, basi waaminini, kwa kuwa niko pamoja nao; yasipotimia, basi wao—wao sio. Ni manabii wa uongo.” Yeye alisema, “Lakini, kuyachunguza, kuona kama yatatimia.”

246 Sasa angalieni. Kama . . . Mungu Yule aliyenena katika nabii mtakatifu, alinena kuhusu kuja kwa Masihi, kwa ajili ya utukufu na heshima ya Mungu.

247 Kama ningalijua ni nani atakayekuwa rais kwenye msimu ujao wa kupukutika majani, na ningelitangaza, huo ungekuwa ni unabii. Hiyo ni kweli. Lakini Mungu hatabiri namna hiyo, kuninii tu, loo, kuwa tu akicheza. Mungu hufanya jambo la kumtukuza Yeye. Mnaona?

Lakini Masihi alipokuja, na wakati Masihi alipoondoka . . .

248 Ninataka kuwaulizeni, ninyi nyote Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki, Lutheri, Pentekoste, Nazarayo, Pilgrim Holiness, ninyi nyote. Nataka kuwaulizeni jambo fulani. Hivi hamfikirii ya kwamba Mfalme huyo wa manabii, Yesu, angalijua jinsi ya kulianzisha Kanisa Lake Mwenyewe? Ikiwa manabii wote walinena habari Zake, na kumwelekezea Yeye, ni Kanisa la namna gani aliloanzisha? Wakati alipoondoka, Yeye alisema . . . Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alimwambia Petro, “Juu ya ufunuo wa Neno la Mungu,” alisema, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Hiyo si ni kweli? Vema. Wakati alipokuwa . . .

249 Kabla Yeye hajaondoka, katika Marko 16, Yeye alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Je, Yeye alisema hilo? "Katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watashika nyoka, watakunywa vitu vya kufisha." Yeye pia alisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." Hiyo ni kweli? Hizo ndizo ishara ambazo zinapaswa kulifuata Kanisa Lake. Sio dhehebu. Ni shirika lililoanzishwa lililowekwa na Mungu, likajazwa na Roho Mtakatifu, Kanisa lililozaliwa Mbinguni linalotoka kwenye madhehebu yote, kundi halisi la watu wanaoamini.

250 Wahudumu hawa wanaosimama hapa wako pamoja tu na mimi. Sisi ni wanadamu. Yeye ni Mungu, bali tuko hapa kumwakilisha Yeye. Tuko hapa kuwaambia ya kwamba sisi... Mungu ametutuma kufanya kazi hii, kuwawekea wagonjwa mikono. "Ishara hizi zitafuatana na hao." Ishara hizo, ishara zote ambazo alizungumzia, zitamfuata mwaminio. Hizi hapa, zikifuata. Zinafuata.

251 Wala Mungu hana upendeleo. Yale aliyomfanyia Hattie, atakufanyia wewe. Aliyomfanyia yule kipofu, atakufanyia wewe, kipofu. Anayomfanyia kiziwi, atakufanyia wewe. Lolote alilomfanyia mtu mwingine, atakufanyia wewe, kama tu utaamini. Hiyo ni kweli?

Sasa, Ndugu Teddy, ninakutaka ucheze *Amini Tu*.

252 Basi wakati watu hawa wakipitia mstarini, basi tutaenda upande huo mwingine. Tutapita, sisi sote tukiwawekea mikono, tukiwaombea, kwamba magonjwa yenu yaponywe. Nayo yanaweza. Yataponywa. Wala sijui yale Mungu atakayofanya. Nimesimama tu papa hapa sasa hivi, bila kujua la kufanya. Nitawaombea tu wagonjwa kama nilivyomwahidi mtu fulani ya kwamba ningefanya. Kuwaombea tu...

253 Jumapili iliyopita, kumbukeni, niliwaambia. Jumapili iliyopita ilikuwa ni—ilikuwa ni funuo, na kadhalika. Jumapili hii ningewaombea wagonjwa.

Na tuombe sasa.

254 Bwana, tumesimama hapa kama watumishi Wako. Tumesimama mbele ya watu Wako. Tuko hapa. Hatujui yale utakayofanya. Huenda ukanena kwa lugha. Huenda ukafasiri. Huenda ukatoa ono. Huenda ukanifanya kushika mkono wa mtu fulani, kwa ajili ya ufunuo. Huenda ukanena na kutoa mamlaka, ya, "Sema lolote utakalo." Sijui utakalofanya, Bwana. Na labda unataka tuwawekee wagonjwa mikono. Hatujui ni kitu gani. Tunataka tu kukufurahisha Wewe, Bwana. Tumesimama hapa, kama watumishi Wako. Na hawa ni watu Wako, nasi tunajaribu kuwasaidia, kulingana na vile Neno Lako linavyosema tufanye. Tunajaribu kuyafuata maagizo Yako. Nami ninakuomba Wewe, Bwana, ya kwamba utatupatia tunayohitaji, kuwahudumia hawa watu, kupitia Jina la Yesu Kristo. Amina.

255 Ninawataka ninyi wengine wote mwinamishe kichwa chenu na kuomba. Wakati Ndugu Wood, tafadhali . . .

256 Na, ndugu wahudumu, ninaamini tungesimama papa hapa juu. Ni wangapi waliopo? Ninyi wanne hapa? Vema. Wawili kila upande pale, nami nitasimama papa hapa mwishoni mwa mstari, papa hapa. Mnaona? Dakika moja tu. Sasa, zunguka moja kwa moja, uje hapa, ndugu, mpendwa. Sasa, jambo ndilo hilo, simama moja kwa moja hapo sasa, nao watapitia hapo. Kusanyiko lote . . . Sasa, iwapo ninyi wavulana wadogo mngesogea nyuma kidogo, wapate kupita.

257 Sasa, wakati sisi sote tukiomba, nendeni moja kwa moja kwenye viti vye—vyenu basi. Katika dakika chache, nitaita upande huo mwingine.

258 Sasa, kila mmoja wenu, sio tu wahudumu, bali, ninyi nyote mnapaswa kuwaombea watu hawa. Hujui yale Mungu anayoweza kukufanyia wakati ukimwombea mtu mwingine. Vipi kama ungesema jambo linalofaa? Vipi kama . . . Huyu hapa mwanamke amesimama hapa, ambaye ni mgonjwa sana inawabidi kumshikilia. Vipi kama maombi yako yangekuwa ndiyo jambo linalofaa, kama tu vile Banks alivyosema jambo linalofaa, kama Hattie alivyosema jambo linalofaa? Vipi kama wewe ungesema jambo linalofaa, maombi yako, kumfanya Mungu ashuke na kufanya jambo fulani? Mnaona, huyu si mtu mmoja tu. Hili ni Kanisa la Mungu aliye hai, kila mtu. Mnaona? Sasa, kila mtu awe katika maombi.

259 Sasa, huyu ndiye? Ndugu Banks, wewe wapitishe tu watu. Mtu fulani na asimame *hapa* ndani, tafadhali. Yuko wapi mmoja wa mabawabu? Ndugu Byrd, utawasaidia kupita, basi. Ndugu Banks, wewe njoo hapa, basi, tafadhali, hapa.

Na tuombe.

Bwana Yesu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . .

260 Naam, endelea kuwaleta sasa. Naomba waponywe, tunapowawekea mikono! . . . ? . . .

Njoni moja kwa moja mbele sasa. Kila mmoja wenu, ombeni sasa! . . . ? . . .

261 Katika Jina la Yesu Kristo . . . ? . . . Katika Jina la Yesu Kristo, tunaweka mikono . . . ? . . .

Tuna furaha sana kuninii . . . ? . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . .

262 Waponye wagonjwa na wanaoteseka, mahali mbalimbali. Na jalia wabarikiwe, Baba, kwa heshima na utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

263 (Sasa hakikisheni . . . ? . . . Ndipo mngekuwa tayari, wakati huo?) Vema. Kama . . .

264 Bwana akubariki, ndugu. [Ndugu huyo anasema, "Bwana akubariki. Nimetoka Sweet Home, Oregon, Ndugu Branham."—Mh.] Vema, kutoka Oregon. ["Nasi tutakuona huko . . ."] San Jose. ["San Jose. Tunaelekea huko."] Vema, ajabu. Mungu akubariki. Natumaini—natumaini utakuwa tu mmoja wa mikutano iliyo mikubwa sana. ["Tunajua utakuwa. Kama Mungu yuko, haina budi kuwa."] Asante—asante—asante, ndugu yangu. Bwana akubariki.

265 Hii si ni kama Mbinguni? Unapowazia, kuihubiri Injili, na watu wakiinua mikono yao kwa Kristo, wagonjwa na wanaoteseka wakipitia mstarini, ibada za ubatizo, ushirika, udugu, hiyo ni—ni sehemu ndogo tu ya Mbinguni imeshushwa ardhini. Mnajua, sisi . . . Ninajisikia kama yule mtume alivyosema wakati ule, "Ni vema kwetu kuwa hapa." Kama tungeweza . . . Hatuhitaji ila Maskani moja. Lakini tunapenda kuwa hapa kwa ajili ya ibada ya Mungu.

266 Sasa, kila mmoja wenu ninyi watu mnaopitia mstarini asubuhi ya leo, aliyeombewa, kumbukeni tu, kwamba Mungu yuyo huyo aliyeyajalia mambo haya yote mliyoyasikia yamefanywa kote nchini, nayo ni ya kweli, kweli tu yawezavyo kuwa. Nao wahudumu hawa wote hapa, na yale ambayo yamefanywa katika huduma yao, yale ambayo yamefanywa katika huduma ambayo Bwana amenipa, tumesimama hapa kwa uaminifu, kwa mioyo yetu yote, tukiomba, tukiwawekea mikono, vile hasa tu Yesu alivyosema. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa ni ninii tu . . . Kuna jambo moja tu la kulizuia lisitendeke, hilo lingekuwa ni ninyi kutokuliamini.

267 Yesu alisema, "Njoni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na mliolemewa na mizigo mizito, nitawapa raha. Yeyote atakaye, na aje." Sasa kuna njia moja tu kwenu kulikosa. Neno la Mungu ni kweli. Njia moja kwenu kulikosa, ni kutokuja. Hiyo si ni kweli? Hiyo ndiyo njia ya nyinyi kulikosa.

268 Mungu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Kuna njia moja tu kwenu kulikosa, hiyo ni kutokuliamini. Kama utaliamini Neno la Mungu, Mungu atatimiza Neno Lake. Unaona, kuninii . . . Hilo lingekuwa . . .

269 Hiyo ndiyo ya kwanza, ya mwanzo. Hiyo ndiyo njia ya kuwaombea wagonjwa. Kuwapitisha, kuwawekea mikono, kuwapaka mafuta, ama chochote alichosema Mungu, njia. Lakini baada ya hayo yote, kusudi Mungu akujulishe ya kwamba Yeye yuko miongoni mwa watu Wake, Yeye huonyesha ishara na maajabu. Na, mnaona, ni ishara na maajabu ya Mungu aliye hai, kufanya mambo afanyayo. Sasa, Yeye ni wa ajabu. Hamfikirii hivyo?

270 Sasa ndugu wanafanya matayarisho, mle ndani, kwa ajili ya i—ibada ya ubatizo. Nayo itafanywa tu haraka. Na sasa, wale watakaobatizwa, wanawake nendeni chumbani. Hiyo ni kweli, wanawake mlio *hapo*? Wanawake *hapa*, na wanaume upande *huu*.

271 Tunapojitayarisha kwa ajili ya ibada ya ubatizo, ninataka kusoma Maandiko, katika dakika chache zijazo. Nasi tutaninii . . .

272 Ninajua baadhi ya viungo vyenu hapana shaka vinauma, kutokana na kusimama. Basi iwapo mnaweza kusimama tu kwa dakika zingine chache, mtaona tamasha zuri mtakapoona ku—kule kutumbukizwa kwa watu hawa.

273 Ninataka kusoma baadhi ya Maandiko sasa yanayopatikana katika Kitabu cha Matendo, mlango wa 2, wakati wanapojitayarisha kwa ajili ya ubatizo. Nafikiri kuna yapata tu watu wawili ama watatu watakaobatizwa; haitachukua ila muda mfupi tu. Nami nawatakeni msikilize kwa makini sasa. Nitaanza kusoma kutoka kwenye Matendo 2, kifungu cha 28, kuanzia, kusoma.

> *Umenijulisha njia* ya *uzima*—njia *za uzima* (liko katika wingi); *utanijaza furaha kwa* nyuso *zako*.
>
> *Waume na ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata sasa.*
>
> *Basi kwa kuwa ni nabii, . . .*

274 Ni wangapi walijua Daudi alikuwa ni nabii? Hakika. Alikuwa mtunga zaburi na nabii.

> *Basi kwa kuwa ni nabii,* na ujuzi *ambao Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika* uzao *wa viuno vyake, kulingana na mwili, atamketisha Kristo katika kiti chake cha enzi;*
>
> *Yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala* mwili wake *haukuona uharibifu.*
>
> *Yesu huyu Mungu alimfufua,* hivyo basi *sisi sote tu mashahidi wake.*

275 Hilo si linasikika kama ni leo hii? Sisi ni mashahidi wa mambo haya. Ninaweza kusema, asubuhi ya leo, "Hattie, wengine wenu, sisi ni mashahidi wa mambo haya."

> *Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu . . . akiisha kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona na kukisikia.*

*Maana Daudi hakupanda* mbinguni: *bali yeye mwenyewe* alisema, *BWANA alimwambia Bwana wangu, Keti upande wa mkono wangu wa kuume.*

276 Mnakumbuka Jumapili iliyopita jinsi tulivyozungumza juu ya manabii, wote watu wakuu, jinsi ilivyowabidi kufa? Lakini Mmoja alikuja, Uzao wa kifalme!

*. . . Keti upande wa mkono wangu wa kuume,*

*Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.*

*Basi nyumba yote ya Israeli na wajue* yakini, *ya kwamba Mungu amemfanya Yesu* huyu ambaye nyinyi *. . . mlimsulubisha kuwa Bwana na Kristo.*

*Walipoyasikia haya* (ya kwamba Yesu alikuwa Bwana na Kristo pia); *walipoyasikia haya wakachomwa* mioyo *yao, wakamwambia Petro na . . . mitume wengine, Tutendeje, waume na ndugu zetu?*

*Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa Jina lake Yesu Kristo kwa ondoleo la* dhambi *zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*

*Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa* wote walio mbali, *na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.*

*Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya akisema, jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi.*

Nao *waliolipokea neno lake wakabatizwa: na siku ile wakaongezeka watu wapatao elfu tatu.*

*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na* katika *ushirika, na . . . kuumega mkate, na katika kusali.*

*Kila mmoja akaingiwa na hofu: ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume.*

*Na wote walioamini* walikusanyika *mahali pamoja: na kuwa na vitu vyote shirika.*

*. . . kauza mali zao, na vitu vyote walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja.*

*Nao* sikuzote *kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, . . . wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe,*

*Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*

277 Sasa wakati wakija majini. . .Wewe nijulishe wakati afikapo, aendapo majini.

278 Mpate kujua ya kwamba ile neema kuu hutawala pamoja na Mungu, ninataka kurejea nyuma. Siwezi kabisa kujizuia kuweka kitu kingine ndani. Hivi mlijua, hao wavulana wawili, watoto wa mwanamke huyo waliookolewa, Mungu alijua hilo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu? Nayo majina yao kweli yaliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Biblia inasema hivyo. Nalo ilibidi tu litende kazi katika dakika hii.

279 Hivi mlijua, Mungu alijua ya kwamba tungekuwa tumesimama hapa, miaka milioni kumi kabla ulimwengu haujapata kuanzishwa? Mnajua, Yeye alijua tungekuwa tumesimama hapa, asubuhi ya leo. Kutokuwa na kikomo kwa Mungu kulijua kila nzi, kila kiroboto, kila wakati wangepepesa macho yao, na wangeweza kutoa kiasi gani cha shahamu. Kabla ulimwengu haujaumbwa kamwe, Mungu alijua hilo.

280 Sasa, mnasema, "Vema, kama alijua hilo, basi kwa nini unahubiri?"

281 Huyo ni Mungu, sehemu ya mpango wa Mungu. Kuhubiri ni mpango Wake. Wakati alipowaangalia mitume. . .Yeye aliyaangalia mavuno. Akasema, "Mavuno yameiva, nao wafanyakazi ni wachache. Ombeni Bwana wa mavuno, kwamba atatuma wafanyakazi katika mavuno Yake." Ni wangapi wanaokumbuka hilo? Vema, kwa nini iwabidi kumwomba Bwana wa mavuno, kutuma wafanyakazi katika mavuno Yake, kama Bwana wa mavuno alikuwa amesimama pale, akijua lingetendeka? Kwa nini? Mungu ameupanga sana, kwamba ninii Yake. . .Sasa sikilizeni hili. Mungu ameupanga sana, kwamba mpango Wake hauwezi kusogea pasipo wewe na mimi. Na maadamu hatufanyi yale Mungu anayotuongoza kufanya, tunalemaza mpango Wake. Lakini wakati Kanisa linapotenda kazi kwa upako wa Roho Mtakatifu, basi tuko katika mapenzi ya Mungu, tukitekeleza mpango Wake. Loo! Mara nitakaporudi kutoka California, Bwana akipenda. . .

282 Kile Maskani ya Branham inachohitaji ni uamsho. Amina. Wanahitaji uamsho na kujazwa kwa Roho Mtakatifu. Sasa hiyo ndiyo haja kuu ya maskani hii. Baadhi ya watu wazuri sana ulimwenguni huja hapa, lakini wanachohitaji ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ninahisi hilo, ninaweza kujua. Basi mara tutakaporudi, Bwana akipenda, tutakuwa na uamsho kwa kusudi lilo hilo, kusudi washiriki wa maskani hii, ambapo watu walikuwa wakimtafuta Roho Mtakatifu, waweze kuingia ndani, wapokee maelekezo na kadhalika. Mikutano ya maombi hapa ndani, wampokee Roho Mtakatifu, kusudi kanisa liweze kurudi kwenye mapenzi ya Mungu, na kuendelea mbele na mpango wa Mungu, unapoendelea mbele.

Bwana awabariki. Ninaamini wako tayari sasa kwenye dimbwi.

283 Wewe ichukue hii, halafu nitaenda mle ndani na kuomba pamoja nao...?...

59-1115 Huduma Yangu Mpya
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org